Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 75 No. 185 | RABIUL1/ RABIUL2 1437 AH | JANUARI 2016 | SULH 1394 HS | BEI TSH. 500/=

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Kwa hakika katika umbo la mbingu na ardhi na mfuatano wa usiku na mchana ziko Ishara kwa wenye akili;

Ambao humkumbuka Mwenyezi Mungu wakiwa wima na wakikaa na wakilala kibavu na hufikiria umbo la mbingu na ardhi: Mola wetu, Hukuviumba hivi bure; utukufu ni Wako, basi Utuepushe na adhabu ya Moto. (3:191-192)

Khalifa Mtukufu aeleza falsafa ya mwaka mpya:

Tutathmini kiwango cha taqwa

Na Mwandishi wetu, Dar es Salaam.

Katika hotuba ya Sala ya Ijumaa ya tarehe 1/1/2016, Kiongozi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Duniani Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a. alizungumzia juu ya haja ya kutathimini viwango vyetu vya Taqwa sambamba na mabadiliko ya tarehe.

Akiongea kwenye hotuba hiyo, Huzur a.t.b.a. alisema:

Leo ni siku ya kwanza ya Mwaka Mpya na mwaka huu unaanzia na siku ya baraka, siku ya Ijumaa. Ni utamaduni kutakiana heri ya mwaka mpya, na kwa mtazamo huo watu wanamtumia Hazrat Khalifatul Masih salamu za kumtakia kheri ya mwaka mpya na pia itakuwa wanatakiana heri wenyewe kwa wenyewe. Mwaka mpya unasherehekewa hasa katika ulimwengu wa magharibi au nchi zilizoendelea, kwa tafrija na kunywa usiku kucha na kwa kuwasha fashfashi. Kwa hakika hivi pia ndivyo inavyosherehekewa hata katika nchi za waislamu.



Masjid Baitul Futuh London, Msikiti mkubwa zaidi kwa Ulaya ya Magharibi, ambapo sauti ya Hadhrat Khalifatul Masih a.t.b.a. husikika kila Ijumaa.

Habari za televisheni usiku uliopita zilionesha picha ya jengo la ghorofa 63 lililokuwa likiungua huko Dubai lakini wakati huo huo zilioneshwa sherehe za fashifashi za moto zikirushwa angani na ikaendelea kutangazwa kwa kurejewa rejewa kwamba pamoja na jengo hilo kuungua bado sherehe za fashifashi hazikusitishwa bali ziliendelea. Nchi nyingi za Kiislamu zimo katika mienendo mibaya sana siku hizi lakini hiyo ndio njia ambayo matajiri huonesha mapenzi yao ya dunia. Hata kama ingelikuwa hakukutokea ajali ya moto ilikuwa ni haja ya wakati kwa nchi tajiri za kiislamu kusema kwamba badala ya kupoteza mali katika mambo ya kipuuzi ni vyema sana kuwasaidia Waislamu walioathirika na matatizo mbalimbali. Lakini hiyo ndio hali ya mambo, kiasi hiki kwamba siku chache zilizopita ilitangazwa kwenye habari kwamba hoteli ya kipekee kwa ufahari huko Dubai ilikuwa imejenga mti mkubwa wa Krismas kuliko yote duniani ukigharimu jumla ya dola za kimarekani Milioni 11. Mambo hayo zama hizi ndio vipaumbele vya matajiri wa Kiislamu.

Kwa upande mwingine, kuna Waahmadiyya wengi ambao waliutumia usiku wao wa jana kwa kumuabudu Mwenyezi Mungu au waliamka mapema kwa ajili ya sala zao za sunna kama njia ya kuuanza mwaka mpya. Sala ya Tahajjud ya pamoja pia ilisaliwa katika sehemu kadhaa. Pamoja na hayo yote bado tunaambiwa sisi sio Waislamu lakini wale wasababishao fujo hao ndio Waislamu. Kwa vyovyote vile, kwa fadhila za Mwenyezi

Endelea uk. 3

Amir akutana na Waziri wa Mambo ya Ndani

Na Mwandishi wetu, Dar es Salaam

Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya Tanzania Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry amekutana na kuzungumza na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mh. Charles Kitwanga.

Amir pamoja na ujumbe wake alikutana na waziri Kitwanga hivi karibuni kwenye ofisi za Wizara hiyo zilizopo eneo la Posta Mpya jijini Dar es Salaam.

Sheikh Chaudhry alisema lengo la kukutana na Waziri Kitwanga mbali na kumpongeza kwa dhamana aliyopewa kuiongoza Wizara hiyo pia ni kujitambulisha na kumhakikishia ushirikiano na Serikali.



Amir sahib akiwa ofisini kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mh. Charles Kitwanga wakati alipomtembela ofisini kwake

"Lengo la kuja kukuona ni kujitambulisha na Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya ipo tayari kushirikiana na Serikali", alisema Sheikh Chaudhry.

Alimweleza Waziri Kitwanga kuwa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya inayo kiongozi mmoja wa kiroho Duniani ambaye ni Khalifa Mtukufu wa

Endelea uk. 2

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

Michezo katika ubora wake

Katika kusheherekea ufunguzi wa msikiti mpya na wa kwanza wa Jumuiya ya Waislam wa Ahmadiyya katika jiji la Mbeya. Jumuiya ya Waislam Waahmadiyya tawi la Mbeya iliandaa ligi ya mpira wa miguu iliyoshirikisha timu nane za vijana wa kutoka katika manispaa ya Mbeya mjini na vitongoji wake. Timu hizo ni pamoja na Human Kinetics, Ituha, Zaraguza Ghana, Under 20 Mbeya City, Mbaspo, New Fighter Igonzo, Vijana FC na Mabatini.

Mashindano hayo ambayo yalifanyika kwa takriban wiki 2 yalikuwa na mvuto wa aina yake ambapo vijana wengi walishiriki kwa kucheza ama kushangilia timu zao. Ligi hiyo iliyotambulika kama AHMADIYA CUP ilikuwa na malengo mengi ikiwa ni pamoja na kuongeza ushirikiano miongoni mwa vijana kwani michezo si uadui, vijana kufanya mazoezi ambayo yatawafanya kuwa mbali na mambo yasiyokuwa na maana katika jamii, lakini kubwa kabisa ilikuwa ni kutangaza ujumbe wa Jumuiya kwa vijana hao na jamii kwa ujumla. Ujumbe ambao pamoja na mambo mengine umejikita katika swala zima la amani na ushirikiano katika jamii, kufuata mafundisho sahihi ya Islam, kufuata sunna na Mtukufu Mtume (SAW) yote haya yakibebwa na kauli mbiu "Mapenzi kwa wote Bila chuki kwa yeyote"

Mashindano hayo ambayo yalifikia fainali zake tarehe 27/11/15 ambapo timu za Vijana FC na Mbaspo ndio zilizotinga fainali. Fainali ambayo iliyofanyika katika uwanja wa kumbukumbu ya aliyekuwa waziri mkuu wa zamani Marehemu Edward Moringe Sokoine na uwanja wa nyumbani wa Mbeya City, huku mtanange huo ukirushwa moja kwa moja na kituo cha utangazaji cha Mbeya City FM.

Amir na Mbashiri mkuu wa Jumuiya ya Waislam Waahmadiyya nchini Tanzania, Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry pamoja na mkuu wa wilaya ya Mbeya mjini Mh. Nyarembe D. Munasa kwa pamoja ndio walikuwa wageni rasmi katika kipute hicho. Kama ilivyo kawaida katika mchezo mshindi ni lazima apatikane, ikibidi japo kwa matuta ya penalti au kurusha sarafu juu. Vijana FC ndio walioibuka kidedea kwa kushinda goli 3 kwa 2 za Mbaspo. Hivyo Vijana FC kutangazwa rasmi kuwa washindi wa Ahmadiyya Cup kwa mwaka 2015 na kukabidhiwa kitita cha Tsh 300,000/= ambapo Mbaspo walijipatia kitita cha Tsh 200,000/= zawadi ambazo zilitolewa siku ya ufunguzi rasmi wa MASJID NASIR.

Akimkaribisha mwenyekiti wa chama cha mpira wa miguu mkoa wa Mbeya, ndugu Haroub Suleimani, Sheikh wa mkoa wa Mbeya Karimuddin Shamsi alisema kuwa lengo la jumuiya ni kuonyesha kwa vitendo mafundisho sahihi ya Islam ambayo yanasisitiza amani miongoni mwa jamii. Akasema kuwa Jumuiya imekuwa mstari wa mbele kuhakikisha jambo hili na ndio maana imejenga msikiti mkubwa kwa lengo la watu kufanya ibada na kumcha Mwenyezi Mungu.

Nae Mwenyekiti wa chama cha mpira wa miguu mkoa wa Mbeya, aliipongeza Jumuiya kwa kuandaa na kufadhili mashindano hayo, huku akisisitiza kuwa yawe ni mashindano ya kila mwaka kwani kupita mashindano hayo, kunawezekana kuvumbua vipaji vingi katika siku za usoni, vipaji ambavyo vinaweza kuwa na tija kubwa si kwa mkoa tu bali kwa Taifa kwa ujumla wake.

Akifunga mashindano hayo, mkuu wa wilaya wa Mbeya mjini Mh. Nyarembe D. Munasa aliishukuru sana Jumuiya kwa kuona umuhimu wa michezo katika jamii, akasifu sana mchango wa Jumuiya katika kulinda na kutetea amani miongoni mwa jamii. Pia aliishukuru Jumuiya kujenga msikiti mkubwa mjini Mbeya na kushauri kuwa si vibaya kama itajenga hata na chuo kikuu cha Ahmadiyya mjini Mbeya. Aliomba na madhehebu mengine yachukue mfano wa Jumuiya ya Waislam wa Ahmadiyya katika kufanya jitihada za ustawi wa jamii, katika nyanja za michezo, elimu na huduma mbalimbali za kijamii, ikiwemo shule na hospitali.

Amir akutana na Waziri wa Mambo ya Ndani

Kutoka uk. 1

Tano, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (Mwenyezi Mungu Amsaidie) na imeenea katika nchi takriban 207 duniani.

Alisema kuwa Waislamu Waahmadiyya daima ni wenye kufuata sheria za nchi na kwamba Jumuiya Ahmadiyya kama taasisi haijihusishi na siasa lakini wafuasi wake kueneza mafundisho ya amani inayofanywa na Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya na kwamba kwa upande huo inaisaidia Serikali hususan Wizara yake yenye jukumu la kuhakikisha amani na usalama.

"Naomba niwahakikishie kwamba kazi mnayoifanya ya kuunganisha watu na kueneza amani inaturahisishia kazi yetu, karibuni sana. Kazi yetu ni kuhakikisha kwamba kunakuwepo na amani na usalama. Maendeleo hayaji kama hakuna amani. Mnaleta utulivu wa moyo, nasi tunaleta utulivu wa mwili", alisema.

Amir Sahib alisema kuwa maana ya Islamu ni amani na kwamba ni kwa bahati mbaya sana kwamba mambo yanayofanyika katika nchi nyingine hususan ulipuaji wa kujitoa muhanga na ugaidi yanaupaka matope Uislam na kwamba sio mafundisho ya dini Tukufu ya Islam.

Sambamba na hilo alimweleza Waziri Kitwanga kuwa kwa miaka mitano au sita iliyopita Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya imekuwa ikiandaa mikutano ya amani katika mikoa mbalimbali kuelezea masuala ya amani ambalo limekuwa ndilo jambo nyeti ulimwenguni kwa sasa.

Alisema mwezi Juni mwaka wa jana mkutano kama huo ulifanyika mkoani Shinyanga ambapo viongozi wa Serikali pia walishiriki. Aidha, Jumuiya hivi karibuni imepanga kuaanda mkutano wa amani katika mkoa wa Dodoma.

Akimshukuru Waziri Kitwanga, Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya Tanzania Bw. Seif Hassan alimweleza kuwa Jumuiya Ahmadiyya itaendelea kumwombea na kumtakia heri katika shughuli zake. Vile vile alitumia fursa hiyo kumwalika Waziri Kitwanga ambaye pia ni Mbunge wa jimbo la Misungwi, Mwanza kwenye misikiti yetu iliyopo Nyegezi, Mwanza na hapa Mnazi Mmoja, Dar es Salaam.

Mwishoni, Amir Sahib alimkabidhi Mhe Kitwanga zawadi ya vitabu vya Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya ikiwemo Tafsiri ya Qurani Tukufu kwa Kiswahili pamoja na kitabu cha 'Mauaji kwa jina la Allah' ambacho kinachopinga dhana ya wale wote wanaofanya mauaji na uharibifu kwa kuwaua watu kwa kisingizio cha dini ya Allah.



Amir sahib pamoja na msafara wake wakiwa ofisini kwa Waziri wa Mambo ya Ndani Mh. Charles Kitwanga wakati walipomtembelea ofisi kwake kama sehemu ya kujenga mahusiano mema na viongozi wa Srikali ya awamu ya tano

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Abdurahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Muhammad Arif
Msambazaji: Omar Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Abdullah Khamis Mbanga
2. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu@yahoo.com

Tutathmini kiwango cha taqwa.

Kutoka uk. 1

Mungu sisi tu Waislamu na kwa ajili ya hilo hatuhitaji uthibitisho wa mtu yeyote yule awaye. Iwapo tuna hamu ya kutambuliwa Uislamu wetu kuwa wa kweli basi ni mbele ya uoni wa Mwenyezi Mungu.

Na hili halipatikani kwa kusali sala za nafali za mtu mmoja mmoja au kwa jamaa katika siku ya kwanza ya mwaka au kwa kutoa sadaka au kufanya matendo fulani ya wema. Hakuna shaka kwamba matendo mema huvutia baraka na rehema za Mwenyezi Mungu lakini kuna haja ya kufanya maamuzi ya kweli na ya kudumu katika hilo. Mwenyezi Mungu anapenda kuwe na hali ya kudumu katika wema. Pamoja na kusali sala za Tahajjud, kile kinachotakiwa na Mwenyezi Mungu ni kuleta mapinduzi ya kweli ya uchamungu ndani ya nyoyo zetu.

Jambo hili haliwezi kufikiwa kwa kufanya wema kwa siku chache tu. Hatuna budi tutafakari sana ni njia gani tukizishika zitatupelekea kupata radhi za Mwenyezi Mungu.

Kufikia hapa Hazrat Khalifatul Masih a.t.b.a. alielezea nukuu mbalimbali kutoka kwa yule aliyetumwa na Mwenyezi Mungu katika zama hizi kuwa Masihi Aliyeahidiwa. Nukuu hizi zinafafanua jinsi gani kwa njia ya kudumu mtu ajitahidi katika kupata radhi za Mwenyezi Mungu, ni kwa njia gani kuifanya miezi 12 ya mwaka na siku 365 za mwaka kuwa zenye baraka ya kuvutia radhi za Mwenyezi Mungu

Masihi Aliyeahidiwa a.s. anasema:

Angalieni hali ya dunia! Mtume wetu Mtukufu s.a.w. alionesha kupitia matendo yake na maisha yake na kifo chake na kila kitu chake kwamba kilikuwa ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu. Lakini kwa ajili ya Waislamu wa dunia ya leo, iwapo mmoja wao ataulizwa kama yu Mwislamu, atajibu haraka kwa kusema Alhamdulillah. Maisha ya yule anayedai kumfuata yalikuwa ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu lakini Waislamu wa leo wanaishi na kufa kwa ajili ya dunia hadi mmoja wao anapofikiwa na sekeseke la mauti. Dunia hubaki kuwa ndio lengo lake na utashi wake. Ni vipi anaweza kusema basi kwamba anamfuata Mtukufu Mtume s.a.w.?

Jambo hili linabidi litufanye tutafakari zaidi, msilichukulie kuwa ni jambo dogo. Si kitu rahisi kuwa Muislamu. Msiridhike hadi pale mtakapokuwa watiifu kamili kwa Mtukufu Mtume s.a.w. na mtakapozalisha mwenendo wa maisha ya Kiislamu ndani mwenu.

Iwapo unatambulika kama mwislamu lakini bila ya kutekeleza kwa utiifu basi imani yako ni ganda tu na wenye hekima daima huwa hawaridhiki na maganda na sura za nje. Mwislamu aliwahi kumweleza Myahudi awe Mwislamu. Myahudi akajibu, usiridhike na jina la nje tu. Mtoto wangu nilimpa jina Khalid (Mwenye kuishi sana) lakini alifariki jioni ile ile kabla ya jua kuzama. Basi tafuta ukweli na usifurahie jina la nje tu. Ni udhalilifu kiasi gani mtu kutambulika kuwa yumo kwenye umma wa yule Mtume Mtukufu kabisa s.a.w. lakini anayapitisha maisha yake kama vile ayapitishavyo mtu asiye muumini. Onyesheni mfano wa Mtukufu Mtume s.a.w. katika maisha yenu na jitahidini kufikia hali hiyo. Tahadharini kwamba, iwapo hamna hali hiyo basi ninyi ni wafuasi wa shetani. Kwa kifupi inaweza kueleweka vyema kwamba kuwa mpendwa wa Mwenyezi Mungu linatakiwa kuwa ndilo lengo kubwa kabisa la maisha ya mwanadamu kwa sababu hadi pale mtu atakapokuwa mpendwa wa Mungu, na iwapo mtu hapokei upendo wa Mungu, basi mtu huyo hawezi kupata maisha yenye mafanikio. Na hili haliwezi kufikiwa hadi pale ambapo mtu kwa ukweli na uaminifu kabisa atamtii na kumfuata Mtukufu Mtume s.a.w. ambaye kupitia mfano wake uliobarikiwa alituonesha Uislamu ni kitu gani. Upandeni Uislamu huo ndani mweni ili muwe wapendwa wa Allah (Malfoozat, Vol. II, pp. 187-188)

Masihi Aliyeahidiwa a.s. anasema:

'Uislamu hauruhusu uruhubani. Huo ni kwa ajili ya waoga. Haijalishi ni kwa ukubwa wa kiasi gani muumini anashiriki katika mambo ya kidunia, ushiriki wake ni chanzo cha hadhi yake ya juu ya kiroho kwa sababu lengo lake halisi ni imani. Na dunia na utajiri na mapambo yake ni njia ya kuitumikia imani. Jambo kuu ni kwamba dunia haipaswi kuwa lengo lake la mwisho, badala yake, lengo halisi la kufikia malengo ya kidunia lazima liwe ni kuitumikia imani. Na malengo ya kidunia ni lazima yawe yaliyopatikana kwa njia ambayo itaitumikia imani. Kama vile wakati wa kusafiri mtu anafanya matumizi kwa ajili ya usafiri na baadhi ya matumizi mengine kwa lengo la kufikia mahala aendako. Usafiri na matumizi mengine yanakuwa ni dharura ya lazima. Mtu anapaswa kuitafuta dunia kwa namna hiyo hiyo, kama njia ya kuitumikia imani. ' (Malfoozat, Vol. II, p. 91)

Mola wetu, Utupe wema duniani na wema katika Akhera (2:202), Aya hii pia inatoa kipaumbele kwa dunia. Lakini dunia ipi? 'Mema katika dunia hii' ambayo yatakuwa ni chanzo cha mema ya Akhera. Mafundisho katika dua hii yanaonesha kwa uwazi kwamba muumini lazima akumbuke mema ya Akhera wakati wa kutafuta malengo ya kidunia. Neno 'wema katika dunia hii' inajumuisha njia zote bora za kutafuta dunia ambazo muumini anapaswa kuzipita kufikia malengo ya kidunia. Tafuta malengo ya kidunia kwa njia zote zile ambazo zitakuwa na matokeo mazuri na si njia ambazo zitakuwa ni chanzo cha maumivu kwa binadamu mwingine au chanzo cha fedheha kwa mtu yeyote. Kufikia malengo ya dunia kwa namna hiyo bila shaka inakuwa ni chanzo cha kufikia uzuri katika Akhera. (Malfoozat, Vol. II, pp. 91-92)

'Ni lazima ieleweke nini maana ya jahannamu? Jahannamu moja ni ile ambayo Mwenyezi Mungu, Mwenyewe ameiahidi baada ya kifo na nyingine ni katika maisha haya ya dunia. Kama si kwa ajili ya Mungu Mwenyezi, maisha ya hapa duniani kweli ni moto wa Jehannamu. Mwenyezi Mungu, Mwenye Enzi hamuangalia kwa namna ya kumuondolea maumivu mtu huyo au kumpatia faraja. Msifikirie kamwe kwamba utajiri wa dhahiri au nguvu, mali na heshima au kuwa na watoto wengi inakuwa chanzo cha furaha, ridhaa au utulivu kwa mtu na kwamba mtu huyo anakuwa peponi kwa sababu ya vitu hivyo.

Kwa hakika si hivyo. Kuridhika, kutosheka na utulivu ambavyo ndiyo ujira wa peponi haviwezi kupatikana katika mambo haya. Hali hizo zinaweza tu kufikiwa kwa kuishi na kufa kwa ajili ya Mungu. Kwa hili Manabii wa Mungu (amani iwe juu yao) hasa Ibrahimu na Yakubu walishauri: .... basi msife ila nanyi mmekuwa wanyenyekeao (2:133).

Raha za dunia hii huzalisha uchafu wa uchoyo ambao huongeza tamaa na kiu na kiu hiki hakizimiki kama vile ambavyo mtu anavyotaabika kutokana na ugonjwa mpaka ufikie muda mtu afariki. Moto wa tamaa ya ladha zisizo za lazima ni kama moto wa Jahanamu ambao hauwezi kuupatia moyo wa mwanadamu nafasi ya kupata faraja. Kinyume chake humuacha mtu akisononeka na kufadhaika katika shaka na wasiwasi. Kwa hiyo suala hili wakati wowote halitakiwi kubakia kuwa lisiloeleweka kwa marafiki zangu kwamba mtu hapaswi kuwa kama mwendawazimu na aliyezama katika ulevi wa kupenda mali na vitu au familia kwa namna itakayoweka umbali kati yake na Mwenyezi Mungu.' (Malfoozat, Vol. II, pp. 101-102)

Masihi Aliyeahidiwa a.s. anasema:

'Nimefahamu kuwa' Sifa zote ni za Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa walimwengu wote, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa ukarimu, Mwenye Kumiliki Siku ya Malipo (1:2-4) inathibitisha kuwa mtu ajikuzie sifa hizi ndani mwake, yaani sifa zote za Mungu Mwenye Enzi. Wakati mtu anasema: Wewe pekee Ndiye tunayekuabudu (1:5), yeye lazima aitafute kwa njia ya kuakisi, sifa ya Rububiyyat (Sifa ya Kiungu ya kulea na kuendeleza), Rahmaniyyat (Sifa ya Kiungu ya kuwa Mwenye Rehema), Raheemiyyat (Sifa ya Kiungu ya kuwa mwenye ukarimu) na Malikiyyat (Sifa ya Kiungu ya kuwa Mmiliki). Kima cha ubora wa mtu kimo katika kujipakaza rangi ya Mwenyezi Mungu na mtu asichoke mpaka pale atakapofikia kituo hiki. Kufuatia hali hii, hali ya mvuto huzalika ndani ya dhati ya mtu ambayo inamchukua kumfikisha katika ibada ya Mungu naye hufikia katika ile hali ya: na wanatenda wanayoamrishwa' (16:51) (Malfoozat, Vol. II, pp. 132-133).

Masihi Aliyeahidiwa a.s. pia anasema:

'Nani anayejua kama yeye ataendelea kuishi tangu wakati wa Adhuhuri hadi Alasiri? Hutokea wakati mtu ghafla huaga dunia. Wakati mwingine mtu anaonekana mwenye afya lakini anakufa ghafla. Wazir Muhammad Hassan Khan Sahib alikuwa ametoka kutembea na kwa furaha alikwenda ghorofani. Alikuwa amepanda ngazi kwa hatua moja au mbili tu akajisikia usingizi, hivyo akakaa. Mtumishi wake akataka kumsaidia lakini alikataa. Kisha alipanda tena hatua chache lakini pia akaona usingizi nzito na hapo hapo akafariki dunia. Vile vile, mwanachama wa Bunge la Kashmir, Gulam Muhy ud din naye alikufa ghafla.

Kwa hakika, hatujui ni wakati gani kifo kitatufikia. Hii ndio sababu kwa nini ni muhimu kutokukisahau kifo. Uelewa wa imani ni jambo muhimu ambalo humpatia mtu heshima wakati wa kifo chake. Imeelezwa katika Qur'ani Tukufu: .... hakika tetemeko la saa ile ni jambo kubwa (22:2). Sisi hatukatai kwamba 'Saa' pia inaashiria Siku ya Hukumu, hata hivyo, ina maana ya mateso yaliyopo katika kifo kwa sababu ni wakati wa kukatiliwa mbali kikamilifu na mtu anatengwa na mambo yote aliyoyapenda na aliyovutiwa nayo na aina ya tetemeko la kifo ni lenye kumshinda kana kwamba amenasa ndani ya mtego. Kwa hiyo ni kwa manufaa ya mtu kukikumbuka kifo na dunia na vitu vyake haipaswi kuwa ndiyo kipenzi kwake kwa kiasi cha kumsababishia matatizo wakati wa kuiaga dunia. ' (Malfoozat, Vol. II, pp. 146-147)

Masihi Aliyeahidiwa (amani juu yake) alisema kuhusu kufanya mabadiliko ya kiuchamungu:

'Msiishi maisha yenu bila hofu ya Mungu. Jibidiisheni katika maombi na istighfar na kuzalisha mabadiliko ya ucha Mungu. Si wakati wa kubaki mmeghafilika. Mtu anajidanganya kwa kufikiria atakuwa na maisha marefu. Kifikirieni kifo kuwa ni kitu kilicho karibu. Kuwepo kwa Mungu ni jambo la yakini na mtu yeyote atakeyetoa haki zimhusuzo Mungu na kuwapa wengine kwa njia ya uovu, mtu huyo atafikwa na kifo chenye dhaliliko. Sura Fatihah inataja makundi matatu ya watu. Katika siku za mwanzoni mwa Uislamu kama mtu mmoja angeliritadi, ingeonekana kuwa janga kubwa. Lakini leo watu 200,000 wameritadi na kuwa Wakristo na kwa kujitwalia uchafu wao wanamtusi vibaya sana yule aliye msafi zaidi [Mtukufu Mtume s.a.w.]. Mfano wa watu waliokasirikiwa na Mungu unaoneshwa kupitia tauni. Hawa watafuatiwa na kundi la wale ambao Mungu huwapa radhi zake.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. pia amesema kuhusu uchamungu:

Imekuwa kanuni ya Mwenyezi Mungu, Mwenye Enzi tangu azali kwamba wakati anawakataza watu juu ya tendo fulani ni dhahiri kwamba katika hatima ya watu hao kuna baadhi miongoni mwao wataangukia kwenye kosa la kufanya kile walichokatazwa. Kama vile ambavyo aliwakataza Wayahudi katika Torati kwamba wasibadili maneno ya Mwenyezi Mungu basi hatimae baadhi yao waliyabadili maneno ya Mwenyezi Mungu. Ingawaje Quran tukufu haisemi kwamba msibadili maneno ya Mwenyezi Mungu bali inasema: Hakika Sisi Tumeyateremsha mawaidha haya na hakika Sisi ndio Tuyalindao. (15:10) Kwa hiyo, endeleeni kuwemo katika wale waliozama kwenye maombi ili Mungu Mwenyezi akuingizeni katika kundi la wale ambao Amewapa radhi zake. ' (Malfoozat, Vol. II, pp. 265-266)

'Kwa hakika waaminio wanapewa dhihiriko la Mungu na wanakuwa chini ya ulinzi wa Mungu. Lakini kinachohitajika ni kwamba mtu awe kwa dhati ni mchamungu na kusiwe na sehemu yoyote ya ushawishi wa kishetani ndani yake. Mungu hapendi shirk (kumshirikisha Mungu na vingine) na kama mtu ana sehemu yoyote ya ushawishi wa kishetani Mungu Mwenyezi hukihesabu kila kitu chake kwamba chatokana na shetani. Maumivu wanayoyapata wapendwa wa Mungu yanatimia kwa mapenzi yake Mungu. Vinginevyo dunia nzima ijiweke pamoja haiwezi kuwapatia maumivu hata kidogo.

Kwa sababu watu hawa ni mfano wa kuigwa kwa dunia, hivyo ni muhimu kwamba wao pia waonyeshe mifano ya jinsi ya kuvumilia matatizo. Vinginevyo Mungu Mwenye Enzi anasema kwamba yeye hachukui hadhari juu ya kitu chochote kwa namna anavyochukua hadhari wakati wa kuyachukua maisha ya mpendwa wake. Mungu Mwenyezi hataki rafiki yake aonje maumivu yoyote yale. Lakini wanapewa maumivu kwa sababu ya haja ya kuwabainisha. Humo ndimo ulimo ubora wao kwa sababu maadili yao ya juu wakati wa maumivu hudhihirika wazi. Manabii na marafiki wa Mungu hawafikiwi na maumivu kwa namna kama ile, kwa mfano ya Wayahudi ambao wanadhalilishwa kwa maonyesho ya hasira ya Mungu na adhabu.

Badala yake Manabii wa Mungu, huonyesha mifano ya utendaji wa kijasiri. Mungu Mwenyezi hakuwa na uadui na Uislamu lakini bado Mtume (rehma na amani za Mwenyezi

Endelea uk. 4

Tutathmini kiwango cha taqwa.

Kutoka uk. 3

Mungu iwe juu yake) alibaki peke yake wakati wa vita vya Uhud. Kusudio la hili ilikuwa kudhihirisha ujasiri wa Mtukufu Mtume (rehma na amani za Mwenyezi Mungu iwe juu yake). Yeye alisimama peke yake akiwakabili watu 10,000 kwa kuwa alikuwa Mtume wa Mungu. Hakuna Mtume mwingine yeyote aliyepata nafasi ya kuonyesha mfano huo wa ujasiri. Tunawaambia Wanajumuiya wa Jumuiya yetu kwamba wasijisikie fahari kwa kusali tu, kufunga saumu au kuepuka dhambi kuu kama vile uasherati, wizi n.k; watu wengi wasio Wanajumuiya, bali hata washirikina n.k. wako kama nyinyi katika sifa hizo.

Sifa za wachamungu ziko nyingi, jitahidi kuzifikia hizo. Pandikizeni ukuu wa Mungu katika nyoyo zenu. Mungu anakataa matendo ambayo yana hata chembe ya unafiki. Ni vigumu kuwa Mchamungu. Kwa mfano, kama mtu anakutuhumu kuiba kalamu, kwa nini upate hasira? Kujizuia kwako kunatakiwa kuwe kwa ajili ya Mungu. Hasira yoyote itokanayo na hali kama hizo ni kwa sababu ya ukosefu wa ufahamu wa ukweli. Mtu hawezi kuwa mchamungu isipokuwa awe amepitia hatua nyingi zilizo mfano wa kifo.

Miujiza na ishara ni matokeo ya uchamungu lakini suala kuu ni uchamungu wa kweli. Kwa hiyo, msijali sana kuhusu miujiza na maono, badala yake jitahidi kuufikia utawa. Ni watu wema tu ndio hupata ufunuo wa kweli na ufunuo wowote unaopokelewa bila ya uchamungu si wenye kutegemewa. Unaweza ukawa ni kipimo cha ushawishi wa kishetani.

Msimchukulie mtu yeyote kuwa mchamungu kwa sababu ya kupokea kwake ufunuo, badala yake, uchambueni ufunuo wake kulingana na hali yake ya utawa. Fumbieni macho kila kitu kingine bali kwanza patanisheni hatua zake za Uchamungu. Shikilieni mifano ya Manabii wote wa Mungu. Wote walikuja kwa lengo la kuwafundisha watu njia za uchamungu. ... Walinzi wao wa kweli ni wale tu ambao ni wachamungu (8:35).

Qur'ani tukufu inafundisha njia nzuri za kufikia uchamungu. Sifa bora za Mtume zinahitaji kwamba wafuasi wake pia wawe na sifa bora. Kwa vile Mtukufu Mtume alikuwa Mbora wa Manabii wote (amani na baraka za Mwenyezi Mungu iwe juu yake), alikuwa kilele cha ubora wa sifa zote za unabii. Ubora wake wa utume ulitokana na huku kukwea kwake vilele vya sifa bora za unabii.

Wale ambao wanataka kumfurahisha Mwenyezi Mungu na wajipatie uzoefu wa miujiza kwa njia ya ajabu wanapaswa kufanya maisha yao yawe yasiyo ya kawaida. Wale watu ambao hukaribia kufanya mitihani hufanya kazi ngumu sana na wakati mwingine huugua magonjwa (kama vile kifua kikuu) na kuwa dhaifu katika mchakato wa kujiandaa. Hivyo, kuweni tayari kuvumilia kila maumivu katika kupita mtihani wa uchamungu. Wakati mtu anashikilia kupita juu ya njia hii shetani naye huongeza mashambulizi yake kwa wingi sana.

Hata hivyo, hatua hufikia ambapo hatimaye Shetani hukata tamaa. Hii ni hatua ambapo maisha ya msingi wa mtu hupitia kifo naye huwa chini ya ulinzi wa Mungu. Anakuwa onyesho la Mungu na mwakilishi wa Mungu. Kwa muhtasari, mafundisho yetu ni haya kwamba mtu lazima atumie vipaji vyake vyote na nguvu zake zote katika njia ya Mungu. '(Malfoozat, Vol. II, pp. 301-302)

Masihi Aliyeahidiwa a.s. anasema:

"Ni sharti la lazima kwa wachamungu kupitisha maisha yao katika upole na unyenyekevu. Hili ni tawi la utawa ambalo kupitia hilo ni lazima tupigane vita vya kujiepusha na hasira zisizo za msingi. Wachamungu wengi na wakweli hukutia kwamba kujiepusha na hasira ni hatua yenye changamoto kubwa kabisa. Kiburi na majivuno hutokana na hasira na wakati mwingine hasira yenyewe hutokana na kiburi na kujikweza kwa sababu mtu hujawa na hasira wakati anapoipa nafsi yake upendeleo kuliko wengine. Sitaki watu wa Jumuiya yangu kuwa na tabia ya kuwafikiria wengine kuwa bora au duni kuliko wao wenyewe. Au kujisikia kiburi miongoni mwao au kuangaliana kuwa duni baina yao. Mungu peke Yake Ndiye Ajuaye ni nani Mwenye heshima zaidi na nani dhalili. Hii ni tabia mbaya itokanayo na dharau na kuna hatari kubwa ya dharau kukua kama mbegu ikuavyo na hatimaye kupelekea maangamizi ya mtu binafsi.

Baadhi ya watu ni wingi wa adabu wanapokutana na wale ambao wanawaona ni muhimu na wenye nafasi kubwa lakini kwa kweli lililo muhimu ni kwamba mtu amsikilize kwa upole yule anayeonekana mnyonge, ampokee kwa furaha, aheshimu kile anachosema na asimweleze kitu chochote kwa njia ya mzaha ambacho kinaweza kumpatia maumivu.

Mungu, Mwenye Enzi anasema: ... Wala msiwasingizie watu wenu wenyewe, wala msitushane kwa majina ya kupanga. (49:12). Msiitane kwa majina ya kutukanana, hii ni njia ya waovu. Yule anayewafedhehesha wengine mwenyewe hatokufa mpaka naye afikwe na fedheha sawa na hiyo.

Usimdharau ndugu yako kwani nyote mnakunywa kutoka chemchem hiyo hiyo, ni nani basi ajuaye ni yupi ambaye hatma yake ni kunywa zaidi. Hakuna mtu afikiae heshima kwa kupitia kanuni za kidunia. Katika macho ya Mungu Mwenyezi mwenye uchamungu zaidi ndiye mtukufu zaidi: .... hakika aheshimiwaye sana miongoni mwenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni yule amchaye zaidi katika ninyi. '(49:14) (Malfoozat, Vol. I, p. 36)

Masihi Aliyeahidiwa a.s. amesema:

Vipaji vyote alivyotupatia Mungu Mwenye Enzi havifai kupotezwa, bali vinatakiwa vikuzwe na kutumika kwa njia na namna iliyo sawa. Inasemwa: Hakika wamefaulu waaminio. (23:2) na baada ya kufafanua maisha ya wachamungu inasemwa katika hitimisho: ... na hao ndiyo watakaostawi (3:105). Yaani wale wote wanaoshika uchamungu huamini katika ghaibu.

Wanajipoteza katika sala lakini kisha wanaporejea katika hali yao ya kawaida wanatumia katika njia ya Mwenyezi Mungu yale waliyoruzukiwa. Pamoja na uwezekano wa madhara binafsi wao kwa kudumu huamini katika vitabu vya Mwenyezi Mungu vilivyopita na vilivyopo na hatimae wanafikia kwenye daraja la imani ya yakini. Hao ndio watu walio kwenye njia iliyonyooka. Wapo kwenye njia iliyonyooka sawa na ambayo humfikisha mtu kwenye kituo cha mafanikio na ufaulu.

Hawa ndio watu waliofanikiwa ambao hufika safari yao salama huku wakiwa wameokolewa na mashaka ya safari. Hii ndio sababu Mungu Mwenye Enzi ametupatia mafundisho ya uchamungu mwanzoni tu mwa kitabu chake ambacho kimebeba mwongozo kwa wachamungu.

Hivyo Jumuiya yetu inapaswa kuweka mkazo na kuwa na wasiwasi zaidi kuliko wasiwasi wa kitu kingine chochote cha kidunia, kama wao kweli wanao uchamungu au la! (Malfoozat, Vol. I, p. 35)

'Iwapo mnataka kupata mafanikio katika dunia hii na ijayo na kushinda juu ya mioyo basi pitisheni maisha yenu kwa usafi. Tumieni ufahamu wenu vizuri na fuateni amri za neno la Mungu. Jiboresheni na jiendelezeni wenyewe na pia muwe mfano mzuri wa kuigwa kwa wengine. Kisha ni hapo tu peke yake ndipo mtakuwa wenye kufanikiwa; basi ikuzeni mioyo yenu. Iwapo mnataka kuiathiri mioyo basi kuzeni nguvu ya utendaji kwa sababu bila nguvu ya utendaji nguvu tu za maneno au nguvu za mwili haziwezi kufanya kitu chochote. Kuna mamia na maelfu ya watu waongeaji. Wengi wanaitwa Maulawii au Maulamaa ambao husimama juu ya mimbari na baada ya kujipa wenyewe vyeo vikubwa, wao kutoa hotuba. Wanasema achaneni na kiburi, majivuno na matendo mchafu. Hata hivyo, thibitisha utekelezaji wao na utendaji wao wenyewe kutokana na ukweli kwamba ni kwa kiasi gani maneno yao yanauthiri moyo wako! ' (Malfoozat, Vol. I, p. 67)

Kama watu hao wangekuwa na nguvu ya utendaji na wangetekeleza wao wenyewe kabla ya kuhubiri, kungekuwa na haja gani basi ya kuelezwa katika Qur'ani Tukufu: 'mbona mnasema msiyoyatenda? (61: 3). Aya hii inaeleza kwamba kulikuwa na watu katika dunia hii ambao walihubiri yale ambayo hawakuwa wakiyatenda, kama vile ambavyo kwa ukweli kabisa kuna watu kama hao siku hizi na watakuwepo pia katika siku zijazo. ' (Malfoozat, Vol. I, p. 67)

'Sikilizeni ninachosema na kizingatieni kwa makini kwamba kama maneno ya mtu hayatoki moyoni na kama hana nguvu ya utekelezaji, basi maneno yake hayatakuwa na athari yoyote. Hili ndilo linalothibitisha ukweli mkubwa wa Mtume wetu (rehma na amani za Mwenyezi Mungu iwe juu yake) kwa sababu namna ya mafanikio aliyoshinda juu ya nyoyo hayana mfano wake katika historia ya mwanadamu. Na haya yote yalitokea kwa sababu kulikuwa na kuafikiana kamili kati ya maneno yake na matendo yake. ' (Malfoozat, Vol. I, pp. 67-68)

Masihi Aliyeahidiwa a.s. pia amesema:

'Shida nyingine kubwa inayowakabili watu wenye elimu siku hizi ni kwamba wao hawana uelewa kuhusu elimu ya dini. Wakati wanaposoma ukosowaji wa mwanasayansi au Mwanafalsafa, wao huendeleza mashaka na wasiwasi kuhusu Uislamu. Hii huwaongoza kwenye Ukristo au udaharia. Katika hali kama hizo wazazi wao pia wanakuwa hawakutenda sawa katika kutimiza majukumu yao kwa maana kwamba hawakuwapatia muda wowote wakati wote ili kupata elimu ya dini bali wakawashirikisha sana tangu mwanzo katika shughuli ambazo ziliwanyima imani safi. ' (Malfoozat, Vol. I. uk. 70)

'Nimeshasema mara nyingi kabla juu ya kupendana na kushikamana katika Jumuiya. Basi kuweni wenye kuheshimiana na kuwa kitu kimoja. Mungu, Mwenye Enzi ametoa mafundisho kwa Waislamu ya kuwa kitu kimoja vinginevyo nguvu zao zitapungua. Hekima ya kusimama bega kwa bega wakati wa Sala ni kukuza umoja na mshikamano ili upendo uweze kupenya kama umeme kutoka mtu mmoja hadi mwingine. Kama mtakuwa na magomvi na mkakosa umoja mtakuwa mlioshindwa. Mtukufu Mtume (rehma na amani za Mwenyezi Mungu iwe juu yake) alisema pendaneni kila mmoja na ombeaneni kwa siri. Kama mtu anaomba kwa ajili ya mwingine kwa siri basi malaika nao humuombea mtu huyo kama hayo kwa ajili yake. Ni la ajabu kiasi gani jambo hili. Kama maombi ya mtu hayakubaliki basi bila shaka maombi ya malaika ni yenye kukubalika. Ninawashauri na ninataka kuwaambia kwamba msiwe na magomvi baina yenu.

'Nimekuja na mambo mawili tu. La kwanza ni kushikilia Umoja wa Mungu na la pili ni kuonesha upendo na maelewano kwa kila mmoja. Kuweni mifano bora kwa namna itakayokuwa miujiza hata kwa wengine. Hii ndio imani iliyojengwa ndani ya Maswahaba (Mwenyezi Mungu awe radhi nao). na kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu iliyo juu yenu mlipokuwa maadui naye Akaziunganisha nyoyo zenu, hivyo kwa neema yake mkawa ndugu; (3: 104). Kumbukeni kubaki wamoja ni muujiza. Isipokuwa kila mmoja wenu apende kwa ajili ya nduguye kile anachokipenda kwa ajili ya nafsi yake, mtu huyo hayumo katika Jumuiya yangu. Mtu huyo yumo katika taabu na msiba.' (Malfoozat, Vol. II, 48 p.)

Masihi Aliyeahidiwa a.s. amesema:

'Inshaa Allah Jumuiya ya wachamungu itatokana nami. Je kuna sababu gani ya ugomvi na kutoshikamana? Ni uovu, kujiona, kujipenda na matamanio. Nimesema kuwa hivi karibuni nitaandika kitabu na ndani yake nitawafukuza wale wote ambao hawawezi kudhibiti hisia zao na hawawezi kuishi kwa nia njema na kwa umoja. Wale ambao wameelekea njia hii wanapaswa kuelewa kuwa hawataweza kudumu kwa muda mrefu labda wao waonyesha mfano mzuri.

Sitaki nipate kuona aina yoyote ya kukosolewa binafsi kutokana na mtu mwingine. Mtu ambaye halingani na matakwa yangu lakini yumo katika Jumuiya yangu yeye ni kama tawi kavu. Ni nini kingine mtunza bustani anaweza kukifanya zaidi ya kumkatilia mbali? Tawi kavu linafyonza maji pamoja na matawi mabichi lakini mtunza bustani hawezi kulifanya hilo kuwa la kijani. Kwa kweli tawi kavu linayavuta matawi mengine yaanguke chini. Hivyo shikeni maonyo. Mtu ambaye hawezi kujisahihisha mwenyewe hawezi kukaa pamoja nami. ' (Malfoozat, Vol. II, p. 49)

'Mwenyezi Mungu anasema kwenye Qur'ani Tukufu: ....na Nitawaweka wale waliokufuata juu ya wale waliokufuru mpaka siku ya Kiyama; (03:56). Ahadi hii yenye kutia utulivu ilifanywa kwa mwana wa Mariamu aliyezaliwa Nazareth. Lakini mimi ninakupeni bishara njema kwamba Mungu, Mwenye Enzi pia Ametoa bishara njema kwa maneno kama haya wakati akiongea na mwana wa Mariamu aliyetakiwa kuja kwa jina la Masihi.

Fikirini, sasa ni vipi wanatakiwa wawe wale ambao wanataka kuwa pamoja katika bishara hii kubwa kwa kuungana pamoja nami, je ni wale ambao wapo katika hatua ya 'uchochezi wa uovu' na wanaoshika njia za waovu? Kwa hakika si hivyo.

Endelea uk. 5

Tutathmini kiwango cha taqwa.

Kutoka uk. 4

Wale ambao kweli wanathamini ahadi hii ya kweli ya Mungu Mwenye enzi na ambao hawayachukulii maneno yangu kama hadithi za kutunga, wakumbuke na kusikiliza kwa ikhlasi. Kwa mara nyingine tena ninaongea na wale ambao wanahusiana nami na hii si kwa njia ya maungano ya kawaida, bali ni maungano makubwa. Athari ya maungano haya haishii kwangu tu bali inafika kwa Yule Dhati aliyenipeleka mimi kwa yule mheshimiwa, mtu mkamilifu ambaye alileta roho ya ukweli na uaminifu duniani.

Ingelikuwa suala hili linanihusu mimi tu, wala nisingekuwa na wasiwasi au shaka yoyote. Lakini hali haiko hivyo. Athari yake inafika kwa Mtume (rehma na amani za Mwenyezi Mungu iwe juu yake) na kwa Mungu Mwenyezi Mwenyewe! Hivyo, katika hali kama hiyo, sikilizeni kwa makini zaidi kama mnataka kuwa washiriki katika bishara hii na iwapo mnataka kuwa wachangiaji wake na mna kiu ya kweli kwa mafanikio hayo makubwa (kwamba mtakuwa washindi juu ya makafiri mpaka Siku ya Malipo). Nasema tu kiasi hiki kwamba mafanikio haya hayataweza kuonekana barabara mpaka pale mtakapobadilika kutoka kwenye hali ya kulaumiana hadi katika hali ya amani.

Mimi sitosema lolote zaidi ya hili kwamba ninyi mnahusiana na mtu yule ambaye ameteuliwa na Mungu. Basi sikilizeni maneno yake kwa mioyo yenu yote na kuweni tayari daima kuyaingiza katika matendo; hivi kwamba ninyi msiwe kama wale ambao baada ya kukubali wakaanguka katika uovu wa kukataa na wakakabiliwa na adhabu ya milele. ' (Malfoozat, Vol. I, pp. 103-105)

'Hili linapaswa pia kusikilizwa kwa usafi wa moyo kwamba kuna masharti machache kwa ajili ya kukubaliwa maombi. Baadhi yao ni kuhusu mtu ambaye hufanya maombi wakati baadhi ni kuhusu mtu ambaye anaomba kufanyiwa maombi. Ni muhimu kwa mtu ambaye anaomba kufanyiwa maombi kwamba yeye aendelee kuwa na mtazamo wa hofu ya Mungu Mwenye Enzi na alete upatanishi na kumuogopa Mungu katika njia zake zote. Yeye lazima Amridhishe Mwenyezi Mungu kwa uchamungu na uaminifu.

Katika hali hiyo mlango wa kukubaliwa maombi hufunguliwa. Kama mtu anamchukiza Mungu Mwenye enzi na yumo katika kukinzana Naye, ufisadi wake na njia zake zisizo sahihi huwa kikwazo katika kukubalika kwa maombi na mlango wa kukubaliwa maombi hufungwa kwa ajili yake. Ni muhimu kwa marafiki zetu kutoruhusu maombi yetu kupotea bure na kutokujenga vikwazo vyovyote katika njia yao ambavyo vinaweza kuundika kutokana na matendo yao machafu. ' (Malfoozat, Vol. I, p. 108)

'Kinachotakiwa ni kushika njia ya uchamungu kwa sababu uchamungu peke yake ndicho kitu ambacho kinaweza kuitwa kiini cha Shariah. Kama Shariah ilikuwa ielezwe kwa ufupi, basi msingi wa Shariah unaweza tu kuwa uchamungu. Kuna hatua nyingi na daraja nyingi za uchamungu. Hata hivyo, kama mtafuta anazipita hatua na ngazi za mwanzo kwa ukweli na kwa kujituma kwa uaminifu, kutokana na uaminifu wake na ikhlas yake katika kutafuta, anafikia kwenye daraja za juu.

Mungu Mwenye Enzi Anasema: Mwenyezi Mungu Huwapokelea wamchao tu. (5:28). Hiyo ni kwamba, Mwenyezi Mungu, Mwenye Kutukuka anasikiliza maombi ya wachamungu. Hiyo ni ahadi yake. Na ahadi zake hazivunjwi, kama Anavyosema: Hakika Mwenyezi Mungu Havunji miadi.' (13:32). Hivyo, kwa vile hali ya uchamungu ni sharti la lazima kwa kukubaliwa maombi, Je mtu hatokuwa mjinga iwapo anatarajia kukubaliwa maombi yake wakati anabaki kuwa mzembe na anayepotea njia? Kwa hiyo ni muhimu kwa ajili ya Jumuiya yetu kwamba kadri iwezekanavyo kila mmoja wao akanyage njia za uchamungu ili waweze kujipatia uzoefu wa mnyakuo wa kukubaliwa maombi na ili waendelee kukua katika imani. ' (Malfoozat, Vol. I, pp. 108-109)

Masihi Aliyeahidiwa a.s. anasema,

Msidhanie kwama Mwenyezi Mungu anaridhika kwa kufanya baiat tu. Hili ni ganda tu waila kiini kimo ndani yake. Sawa na kanuni nyingi za maumbile kuna maganda ambayo ndani yake huwa kuna kiini. Ganda huwa halina maana bali ni kiini kilichomo ndani ndicho kitumikacho. Hivyo hivyo mtu adaie kufanya baiat na kudai kuwa na imani lakini hana kiini cha mambo haya yote ndani mwake ni lazima atishike na hali hiyo. Muda si mrefu hata kugongwa kidogo tu kunaweza kumfanya kuwa chembecheme na kutupiliwa mbali.

Hivyo hivyo, yeyote yule anayedai kufanya baiat na kushika imani inambidi kuikumbatia na kujiangalia iwapo ameshikilia ganda tu au kweli ameshika kiini. Hadi pale kitakaposhikwa kiini, mapenzi ya imani, utii, baiat, kutegemea na ufuasi; mfuasi wa Islam hawezi kuwa mfuasi wa kweli. Kumbukeni ni kweli kwamba Mwenyezi Mungu mwenye enzi, hathamini ganda bila ya kiini. Kumbukeni sana kwamba ingawaje hatujui mauti yanaweza kumfikia mtu muda gani lakini ni uhakika kwamba kifo kitamfikia kila mmoja. Hivyo msiridhike na madai ya mdomo tu na kulifurahia hilo. Ni ukweli kwamba si jambo la manufaa hadi pale mtu atakapoingia kwenye hali mbalimbali za mfano wa kifo na iwapo hajapitia hali mbalimbali za mabadiliko, hawezi kuona lengo la kweli la ubinadamu. (Malfoozat, Vol.II, p. 167).

Mwenyezi Mungu atujaalie tuyafume maisha yetu sawa na matarajio ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. na tusonge mbele kuuelekea utawa. Tusiyafanye maombi ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. kuwa ni kitu kilichopotea bure, badala yake daima tubakie kuwa wapokeaji wa baraka za maombi ambayo aliyafanya kwa ajili ya Jumuiya yake. Huzur Aqdas alimtakia kila mmoja wetu baraka na kheri ya mwaka mpya, na kwamba Mwenyezi Mungu aufanye mwaka 2016 kuwa ni mwaka wa baraka nyingi na mafanikio kwa kila mmoja wetu na Jamaat kwa ujumla.

Mwisho

Tumepoteza Lulu

Sheikh Chaudhry Inayatullah Ahmad

Na Al-Ustadh Khamisi Sultan
Wamwera, Dar es Salaam

Ni tarehe 24/12/2015 mnamo saa 8:15 za mchana, napokea simu kutoka kwa Mhariri Mkuu wa gazeti la Mapenzi ya Mungu Muadhamu Mahmood Hamsin Mubiru, akinitaka niandike chochote ninachojuwa kuhusu Maulana Sheikh Inayatullah U. Ahmad aliyefariki mjini London –Uingereza tarehe 09/12/2015.

Sheikh Inayatullah ni Mbashiri wa miaka mingi katika nchi yetu ya Tanzania na baada ya kazi hiyo yenye heshima kubwa alistaafu na kwenda kuishi Uingereza. Basi, mimi baada ya kupokea wito wa Mudiri wa Mapenzi ya Mungu, kwa kweli sikumaizi mara moja nianzie mahala gani. Lakini Mungu si Uthmani. Bali ukweli ni kwamba Sheikh Inayatullah Ahmad kwa miaka mingi aliishi na kushughulikia ubashiri mkoa wa Tabora na Mwanza pamwe na wilaya zake. Sehemu hizo Sheikh wanamjua na wanamuelewa. Watakaposikia khabari za kuondoka kwake hapa duniani kwa hakika watasikitika sana. Kama tunavyosikitika sisi. Hili halina shaka kwamba Sheikh Inayatullah alijulikana sana ukanda wa magharibi kwa sababu kule amekaa miaka mingi sana Tabora, Mwanza, Bukoba na Kigoma. Walimuelewa yeye ni mtu mtaabadi na mwanadini. Wale waliopitia Tabora skuli hawakosi kumfahamu, kwa sababu mara kwa mara Sheikh alikuwa anaenda kule kuzungumza na wanafunzi kuhusu mafundisho ya Kiislam juu ya mambo mbalimbali kwenye vuguvugu la siasa, Sheikh aliwasaidia sana wanasiasa. Aliwapa na kuwaonesha mbinu hii na ile ya kudai uhuru. Ni mmoja kati ya wale walioshauri chama cha TANU kwa wakati ule ikubali upigaji wa kura tatu. Mwafrika, mzungu na mhindi. Mawazo hayo kwa hakika yalisaidia sana kwa chama kupata ushindi ambao uliharakisha kupata uhuru kwa muda mfupi. Tendo hilo ni miongoni mwa milolongo ya mambo mengi ambayo Sheikh alikuwa anaishauri Serikali. Kwa kuwa wengi wa wananchi kwa wakati ule waliounda serikali walipitia Tabora skuli, Mwenyezi Mungu Alikuwa Anatia nguvu Fulani katika ushauri wake aliokuwa anautowa kwa chama na serikali.

Wakati nchi hii, mnamo mwaka 1961 inapata uhuru wake, Sheikh Inayatullah hakusahauliwa hata kidogo. Alikuwa miongoni mwa wageni mashuhuri walioalikwa kwenye sherehe hiyo tukufu. Naam, katika miaka ya 66, 66 hivi Sheikh Inayatullah Ahmad aliletwa Dar es salaam kuwa Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Ahmadiyya Tanzania. Alhamdulillah kwa fadhila za Allah, kwa bahati njema kwa miaka ile, nami nilikuwa mtumishi wa Jumuiyya. Basi tukajumuika kufanya kazi pamoja. Hapo ndipo nilipoanza kumfahamu vizuri sana Sheikh Inayatullah ni nani. Hapana shaka ni mtu kama mwingine yeyote, lakini mimi nasema ipo tofauti katika juhudi ya kumwendea Mwenyezi Mungu. Wapo wanaoelekea kwake kwa kukwawa, wengine kwa kutaataa na wapo waendao kwa kusuasua, wengine mwendo wa haraka na wengine kwa mwendo wa mbio. Ndivyo hivi tulivyo.

Sheikh Inayatullah Ahmad alikuwa mwembamba na ni mrefu wa kimo, aliyependa kushika fimbo mkononi mwake kila atakapo kwenda nje. Alimaridadi na mtanashati. Alikuwa m wenye busara na hekima kubwa. Alikuwa mwenye sauti nzito yenye kupenya kwenye masikio ya asikilizaye. Maneno yake huvuta akili ya amsikilizae. Sina shaka, twabiya yake nina hakika daima itamuathiri atayekuwa pamoja naye. Alikuwa anajitahidi asiende kinyume cha mafundisho ya Qur'an Tukufu, mafundisho ya Kiislam. Hakuwa na kigugumizi, bali alikuwa faswaha wa maelezo. Alipenda mno kuzungumza mambo ya dini kuliko kitu kingine chochote. Kalima yake ilikuwa ya unyofu na upole. Binafsi alinipenda na kwa haki ya Mungu hakuwahi kuniudhi hata siku moja.

Sheikh Inayatullah Ahmad hakujali sana elimu ya mtu, rangi au umaarufu, waila alimpa heshima kila mtu. Hata wapinzani wa Jumuiyya ya Ahmadiyya walikuwa wanastaajabu sana. Kwa kweli alikuwa na twabiya na khulka njema za Kiislam.

Allahu Akbar, Sheikh Inayatullah Ahmad alikuwa mwenye sura na wajihi wa bashasha na tabasamu wakati wote umuonapo. Hapa niseme kuwa Sheikh alikuwa anaheshimu sana wakati, khasa wakati wa swala. Wakati wa swala ulipofika tu, alikuwa anamkumbusha msema adhana. Mara nyingi kwa mboni ya macho yangu nimeona akiwasaidia watu mbalimbali walodhoofulhali bila kujali ni wa dini gani. Sheikh Inayatullah alikuwa mkweli na thabiti wa kauli. Alikuwa mwangalifu wa matumizi hakuwa miongoni mwa wafanyao israfu. Hakujifakharisha kwa chakula wala mavazi. Alikula, kunywa na kuvaa bila kupita kiasi.

Swifa hizi nilizoziona kwake ninashindwa kumpa lakabu. Bali swifa yake kubwa kabisa alikuwa anamtegemea sana Mwenyezi Mungu kwa kila jambo. Ibada ya saumu na Tahajudi ilikuwa kwake ni vitu vya kawaida, kwa hakika alijivisha lile vazi rasmi la ucha Mungu na utawa.

Sheikh alikuwa ni kito cha thamani ya imani. Ni lulu inayopatikana kwenye kilindi kirefu cha mkondo mkubwa wa bahari ya Islam. Lulu hii inastahili iheshimiwe. Kwa sababu ni adimu kupatikana. Sheikh Inayatullah alipenda sana dini na mara nyingi alikuwa anatuomba tumwombe sana Allah Awaongoze watu waje kuingia katika Islam na kujiunga katika Jumuiyya ya Ahmadiyya. Kwa njia hii Sheikh hakuwa mtu wa ofisini. Muda mwingi shughuli za ofisi aliniachia miye naye alikuwa anatoka nje kwa ajili ya Tabligh. Ni Amir na Mbashiri Mkuu lakini alikuwa anaenda kwenye maofisi mbalimbali ya Serikali na ya mashirika ya umma tena kwa miguu shabaha ni kuzungumza na watu kuhusu Uislamu. Katika safari hizo mikononi mwa Sheikh alikuwa anabeba magazeti ya Mapenzi ya Mungu, East African Times na vitabu mbalimbali kwa ajili ya kuviuza.

Nimejaribu kueleza kwa uchache mno kile nilichokiona kwa Sheikh Inayatullah Ahmad, nilipokuwa pamoja naye katika shughuli za dini lakini la kushangaza hili la mwisho. Sheikh alipokuwa hapa Tanzania katika uhai wake, alishirikiana na wananchi hadi tukapata uhuru mnano tarehe 09/12/1961. Kifo cha Maulana Sheikh Inayatullah Ahmad kimetokea tarehe 09/12/2015. Ewe Mwenyezi Mungu sisi ni wako na kwako tutarejea. Mpe makazi mema Sheikh wetu huko peponi. Amin.

Bustani ya Washairi

Hae Msiba Mzito

MATOZI

1 Bismillah nabutadi
Kwa jina lake Wadudi
Pekee twamuhimidi
Mola Alotakasika.

2 Wamilele na idhati
Aloumba samawati
Ametawala wakati
Majini na Malaika.

3 Hanayo haja ya mwana
Hana shida subuhana
Hata nisai hapana
Rabi amekamilika.

4 Hapatwi na usingizi
Kila dakika ni kazi
Ndiye Muumba Azizi
Vitu vinavyotumika.

5 Wasalatu wasalaam
Zishuke kwa Akram
Muhammad Muungamu
Siraja inayowaka.

6 Kawashinda kwa daraja
Yeye ndiye namba moja
Huwezi mpata mja
Wa nambaye kuishika.

7 Bila yeye kutokea
Isingeumbwa dunia
Ndiye khatama nabia
Kisima chenye Baraka.

8 Yeye ndiye chem chemu
Ya maji yalo matamu
Kuyanywa huishi hamu
Ni muhali kukauka.

9 Mafunzo yalo kamili
Yalotoka kwa Jalali
Katuletea Rasuli
Ili tuweze zinduka.

10 Na Masihi Ahmadi
Kaja sawa na ahadi
Kwetu sisi ni zawadi
Twashukuru kutufika.

11 Kwisha kutoa salamu
Kwao wetu waadhamu
Rohoni ninayo hamu
Tozi linalodondoka.

12 Hayauliza matozi
Jambo hino liwe wazi
Ni yanini michirizi
Matozi watiririka?

13 Matozi haya ya nini
Yanayotoka moyoni?
Nipe nijue undani
Jambo lililokufika

14 Matozi haya ya damu
Nipe nipate fahamu
Ili niwape kaumu
Chanzo kino cha shabuka.

15 Ni upi wako ujumbe
Wa ukali kama wembe
Au tamu kama embe
Nipe utoke wahaka.

16 Ukiona ladondoka
Tozi jua patashika
Na baidi limetoka
Penye shida na mashaka.

17 Mwanzo mvua mawingu
Hizo siri za kimbingu
Na mimi kusudi langu
Nijue yalofichika.

18 Matozi nayo yalia
Mazito yalotokea
Yanashindwa jizuia
Huzuni imeghubika.

19 Matozi yaniambia
Ametawafu shujaa
Muhubiri mwenye nia
Kila pembe alifika.

20 Ametuhama ulama
Alokuwa na karama
Na elimu ya kuzama
Wapinzani kuwashika.

21 Kufasiri Msahafu
Kwa lugha yetu shufufu
Alikuwa kwenye safu
Hadi ikakamilika.

22 Alikuwa mchungaji
Si Katoro si Ujiji
Kote aliwafariji
Watoe zao sadaka.

23 Kuwarudisha kundini
Alikuwa furahani
Sote tufate Manani
Hapo alifurahika.

24 Hata ukiwa baidi
Shehe atabisha hodi
Ajue una baridi
Au homa kukushika.

25 Kaondoka muhubiri
Wa neno lake Kahari
Amevuka na bahari
Habari kuzianika.

26 Ofisi nyingi kabisha
Ujumbe kuufikisha
Unaohusu maisha
Ya nuru isozimika

27 Hotubaze za upole
Katu hazina kelele
Nia ni kutibu ndwele
Nyoyo zipate nyooka.

28 Katembeza magazeti
Kwa kila kona ya nti
Ili wale makulati
Ya utamu wa hakika.

29 Aliandika makala
Za mantiki, muwala
Kuzindua walolala
Nao wapate amka.

30 Machimbo ya alimasi
Yaliyojaa nemsi
Ili kumcha Mkwasi
Rabi Alokamilika.

31 Elimu za ndanindani
Elimu zenye yakini
Kachota kwenye madini
Ya Masihi Msifika.

32 Amesambaza vitabu
Kwa furaha ya ajabu
Ili wapate zabibu
Kiu ipate katika.

33 Na haki za binadamu
Katu hakulaza damu
Alipigana dawamu
Wanyonge kuheshimika.

34 Tajiri na masikini
Aliwaweka moyoni
Si usiku si jioni
Nyumba zao alifika.

35 Akala bila matata
Chakula alichokuta
Hata na maji ya kata
Katu hakusema aka!

36 Mtama hadi ulezi
Vyote kwake ni azizi
Usivitaje viazi
Hivyo hakutetereka.

37 Ametawafu mpenzi
Ambaye alituenzi
Tukipatwa na simanzi
Wa kwanza kuhuzunika.

38 Akijua mengi mambo
Bado yamo kwenye tumbo
Yaso sura wala umbo
Kwake yalidhihirika.

39 Alipata ya ghaibu
Bushira zilo twaibu
Zikatimia ajabu
Njozi zikakamilika.

40 Kaona njozi kamili
Mlangoni pana fili
Tena hao ni wawili
Ghafula akaamka.

41 Kumbe hiyo ni bishara
Ya mambo yenye hasara
Yalopandisha hasira
Hadi vita kufumka.

42 Ilikuwa ni habari
Yaashiria hatari
Na ongezeko la shari
Kuigombea mipaka.

43 Mipaka hii ya juzi
Wameweka walowezi
Chimbuko la uchokozi
Bara letu Afrika.

44 Huko mjini Belini
Walizichora ramani
Wakagawa majirani
Jambo kubwa la dhihaka.

45 Watu wa kabila moja
Kukatokea kioja
Wakauvunja umoja
Kabila kugawanyika.

46 Watu walo majirani
Ikatua nukusani
Watu wakawa vitani
Damu ikatiririka.

47 Kumbe vita ya Kagera
Iliyoleta hasara
Na uwingi wa madhara
Amini akapigika.

48 Akiwa Kilimanjaro
Aliweza ona ndaro
Sheikh wetu asokero
Mawinguni katoweka.

49 Kesho redio kunadi
Ametawafu asadi
Sheikh Kaluta Abedi
Duniani katutoka.

50 Alitupenda kwa dhati
Maombi kila wakati
Tuwe watu hasanati
Waja walioongoka.

51 Daima sisi wanae
Wasiojua wajue
Ni kwa nini tusilie?
Muhibu ametutoka.

52. Ukosapo Masijidi
Siku mbili na zaidi
Mara hufanya juhudi
Ili wewe kukusaka.

53 Kipindi cha kutengana
Kuileta tafurana
Utuvu wote hakuna
Roho inapapatika.

54 Mazoea yana tabu
Akitoka mahabubu
Roho hupata adhabu
Isipate pa kushika.

55 Akupendaye mpende
Alinambia Umande
Huvuni hadi upande
Ni kanuni iso shaka.

56 Tanzania ndio kwao
Tazama huo upeo
Hupati siku za leo
Kama yeye kumfika.

57 Kapigania uhuru
Kuiondoa kufuru
Wale waliotudhuru
Hadi tukaweweseka.

58 Kutawaliwa aibu
Wabezwa kama kelbu
Kazi kulinda bawabu
Uko nje wapigika.

59 Unatupiwa makombo
Ufaidicho ni shombo
Angalia hili jambo
Jinsi tulivyoteseka.

60 Wakiitacho mshahara
Kwa hakika masihara
Ni kubwa hino hasara
Weusi kudhalilika.

61 Majina yetu ni boi
Watu wasio na rai
Watu waso na uhai
Thamani ilotoweka.

62 Jambo hili alipinga
Na kusema ni wazanga
Jambo hili la kijinga
Lazima litaondoka.

63 Tarehe tisa disemba
Katawafu wetu mwamba
Roho zetu ziliyumba
Sote tukahuzunika.

64 Ni sheikh wetu Inaya
Tulaya asiye maya
Ahamadi ni hidaya
Aliyotupa Rabuka.

65. Mbingu ikamdhukuru
Ikulu ikaamuru
Mwaka huu kwa uhuru
Hakuna kushereheka

66 Ya Rabbi Mola Manani
Twakuomba muauni
Apate kiti peponi
Daraja la kutukuka.

67 Pokea zake juhudi
Mzawa wa Ahmadi
Apate kubwa zawadi
Mola uso mshirika.

68 Binadamu ni dhaifu
Tumejawa mapungufu
Yarabi Mola Raufu
Mabayaye kuyazika.

69 Mkamilifu hakuna
Ila wewe subuhana
Tunakuomba rabana
Kwako aje pumzika.

70 Amuone Muhammadi (saw)
Na Masihi Ahmadi (as)
Na wengine mashahidi (ra)
Wale waliosifika.

71 Asiwe nao baidi
Wapenzi wako Wadudi
Penye ua la waridi
Apate kusitirika.

72 Kaditama iwe dua
Muumbaji wa dunia
Mikono tunainua
Twaomba kukubalika.

Na Mahmood Hamsin Mubiru
(Wamamba) – Dar es Salaam

NI AI YU AHMADI

1. Sheikh Mustahiki, Ni Ai Yu Ahmadi
Afrika Mashariki, akijulika asadi
Hivi sasa kafariki, karejea kwa Wadudi
Ni Ai Yu Ahmadi, Sheikh wetu kafariki.

2. Mmoja wa ndugu zetu, katika wale mabwana
Walotufikia kwetu, khabari kuelezana
Kuja mjadidi wetu, Ahmad Sayidina
Ni Ai Yu Ahmadi, Sheikh wetu kafariki.

3. Ali nasi kwa miaka, kwa kazi za mahubiri
Sana ameshughulika, kuwakilisha khabari
Za Masihi mtajika, kwa ushahidi mahiri
Ni Ai Yu Ahmadi, Sheikh wetu kafariki.

4. Kienda huku na huko, kwa Tabligh hakika
Kapata misukosuko, bali kweli kaanika
Waloleta sokomoko, kawafedhehi Rabuka
Ni Ai Yu Ahmadi, Sheikh wetu kafariki.

5. Ya Allah Dhuljalali, upokeaye maombi
Mja kwako kawasili, ulifute lake vumbi
Ghufira yake kubali, mghufiriye madhambi
Ni Ai Yu Ahmadi, Sheikh wetu kafariki.

6. Uthamini kazi zake, njema alizozitenda
Mlipe malipo yake, namna unavyopenda
Waila asihenyeke, kazi ngumu kumlinda
Ni Ai Yu Ahmadi, Sheikh wetu kafariki.

7. Usimtiye motoni, kwenye miali mikali
Ibabuwayo butuni, na chote kiwiliwili
Umuingize peponi, kwenye kivuli jamili
Ni Ai Yu Ahmadi, Sheikh wetu kafariki.

Al-Ustadh Khamisi Sultan Wamwera
Kimbangulile –Mbagala Rangi 3
Dar es Salaam.

Naibu Waziri wa F edha ahimiza ushirikiano

Na Mwandishi wetu, Dar es Salaam

Naibu Waziri wa Fedha na Mipango Dk. Ashantu Kijaji (Mb) ameitaka Jumuiya ya Waislamu Waahmadiya nchini kuendeleza ushirikiano na Serikali kwa lengo la kufanya kazi kwa pamoja hususan katika kuihudumia jamii.

Naibu Waziri Kijaji aliyasema hayo hivi karibuni ofisini kwake jijini Dar es Salaam alipokutana na uongozi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanzania.

Dk.Kijaji alisema Serikali ipo karibu na raia wake, hivyo madhehebu ya dini hayana budi kushirikiana na Serikali ili kujenga jamii iliyo bora.

"Tunatakiwa kuimarisha ushirikiano wetu ili tupige hatua, nawakaribisha tufanye kazi kwa pamoja kama jamii", alisisitiza.

Akielezea anavyoifahamu Jumuiya Ahmadiyya, Naibu Waziri huyo alisema kuwa alipokuwa mkoani Morogoro amekuwa akishirikiana na Jamaat na amesifu na kuipongeza kwa huduma inazozitoa kwa jamii ikiwemo huduma za afya kupitia hospitali ya Jamaat Ahmadiyya iliyopo Morogoro.

Mapema Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanzania Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry mbali na kuishukuru Serikali pia alimweleza Naibu Waziri miradi mbalimbali inayofanywa na Jamaat kwa lengo la kuihudumia jamii ikiwemo Shule ya Sekondari ya Ahmadiyya iliyopo Kitonga, Dar es Salaam. Aidha, alimfahamisha Dk. Kijaji ambaye pia ni Mbunge wa Kondoa Vijijini mkoani Dodoma kuwa Jamaat Ahmadiyya ipo mbioni kuanzisha Hospitali katika mkoa wa Dodoma.



Amir sahib akimkabidhi nakala ya tafsiri ya Quran tukufu Naibu Waziri wa Fedha na Mipango wakati alipomtembelea ofisi kwake.

Kuhusu mikutano ya amani, Amir Sahib alimweleza Dk. Kijaji kuwa Jamaat Ahmadiyya imekuwa na desturi ya kufanya mikutano ya aina hiyo na takribani miaka mitatu iliyopita mkutano wa amani ulifanyika mkoani Morogoro na kauli mbiu inayotumika ni "MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE". Alisema Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya duniani inayo Kiongozi wa Kiroho ambaye ni Khalifa Mtukufu wa Tano, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (Mwenyezi Mungu Amsaidie) ambaye pia hivi karibuni alizuru Japan ambapo pamoja na mambo mengine, alisisitiza suala la amani ya dunia, jambo ambalo kwa sasa ndilo linalogonga vichwa mbalimbali vya habari.

Mwishoni, Naibu Waziri, Dk. Kijaji ambaye ni msomi aliyebobea kwenye taaluma ya uchumi, alikabidhiwa na Amir na Mbashiri Mkuu zawadi ya vitabu vya Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya ikiwemo Tafsiri ya Kurani Tukufu kwa lugha ya Kiswahili.

Malezi ya watoto ndio Jihadi muhimu kwa wanawake - Khalifa Mtukufu

Na Jamil Mwanga
Dar es Salam

Kiongozi wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya Duniani, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (a.t.b.a) amesema jihadi iliyo kubwa na muhimu zaidi kwa akina mama ni kuhakikisha kuwa watoto wanapata malezi na elimu bora kwa kuwa ndilo jambo litakalowapatia pepo.

Akihutubia kutoka ukumbi wa akina mama (Lajna Imaillah) katika Mkutano wa mwaka wa Uingereza Oktoba, 21, 2015 kwenye viwanja vya Hadiqatul Mahdi, London ambapo hotuba hiyo pia ilirushwa moja kwa moja na televisheni ya MTA, Huzur (a.t.b.a) amesema kuwa kutokana na thamani waliyonayo wanawake, Mtukufu Mtume Muhammad (S.A.W) amewapa hadhi na heshima kubwa.

Mtukufu Mtume Muhammad (S.A.W) amesema kwamba wote wanawake na wanaume wanamwogopa Allah na wanamwamini Mtume lakini wanaume wao wana daraja moja zaidi ya wanawake. Sambamba na hilo, wakati wa zama za Mtukufu Mtume Muhammad (S.A.W) sahaba mmoja mwanamke alihoji kuwa wanaume wao wanafanya jihadi na wanapata thawabu kwa kufanya ibada zaidi kwa kuwa wanasali Ijumaa, wanahiji.tofauti na wanawake ambao wao muda mwingi hubaki nyumbani kuangalia nyumba na kushughulikia malezi ya watoto.

Hapo Mtukufu Mtume Muhammad (S.A.W) alisema kwamba wanawake kwa kufanya kazi ya kuangalia nyumba, kuwalea watoto na kuwapa elimu bora ili wawe raia wema kwenye jamii hiyo inawafanya wapate thawabu sawa na wanaume wafanyao jihadi. "Kwa kuangalia nyumba ya mumewe kuwapa watoto malezi na elimu, hiyo ni sawa na wanaume wanaofanya jihadi", alisema Khalifa Mtukufu (a.t.b.a).

Hivyo, wanawake wanapewa habari njema kuwa kwa kuwalea watoto watapata thawabu sawa na wanaume.

Alisema katika kila nchi idadi ya wanawake ni kubwa zaidi ya wanaume. Wanawake baada ya kuelimika wamepaza sauti zao ili kulinda hadhi yao. Wanawake katika baadhi ya jamii hulipwa ujira pungufu ya wanaume. Vile vile, hutendewa kikatili na wanaume na matokeo yake asilimia 75 ya ndoa huvunjika.

Huzur (a.t.b.a) alisema kabla ya kudhihiri Mtukufu Mtume Muhammad (S.A.W), wanawake katika bara Arabu walidhalilishwa sana lakini kutokana na nguvu ya kiroho ya Mtukufu Mtume Muhammad (S.A.W) na Baraka ya Islam mwanamke amethaminiwa na kwamba hiyo ndio misingi imara iliyowekwa na Islam.

Wanawake wengi katika nchi zinazoendelea na hata katika nchi zilizoendelea wanakosa hali ya kujiamini na wanaona wanadhalilika. Huzur (a.t.b.a) amesema mwanamke anatakiwa kuwa mwenye kumwamini Mwenyezi Mungu na kwamba wanaume wametakiwa kuwatendea wema wanawake. Hata Mtukufu Mtume Muhammad (S.A.W) alipoulizwa kuwa ni nani kati ya baba na mama anayetakiwa kutendewa wema zaidi alijibu mama yako mara tatu na kisha akasema baba yako. Huzur (a.t.b.a) alisema mama hujitolea na kutaabika zaidi kwa kumlisha, kumwogesha mtoto na hujitolea kuacha starehe zake kwa ajili ya mwanaye.

Huzur (a.t.b.a) aliwataka akina mama kujaribu kuwalea watoto vyema ili wawe raia wema kwenye jamii jambo litakalofanya watoto hao kupata pepo. Alisema mama ndio njia ya kumfanya mtoto kupata pepo kwa kumlea vyema. Mama hutoa huduma zote hizi kwa mtoto sio kwa ajili ya kulipwa chochote bali kwa ajili ya kuwawezesha watoto hao wapate pepo.

Huzur (a.t.b.a) alisema mama na watoto wote wanatakiwa kuelewa jambo hili. Akina mama wasiwaharibu na kuwaua watoto wao bali wazingatie kuhusu elimu na malezi yao.

Akizungumzia kuhusu masuala ya ndoa na malezi ya watoto, Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alisema kuwa ndoa zinapovunjika watoto huathirika kisaikolojia na huanza kubwia dawa za kulevya. Wanawake wawalee watoto wao kwa wema. Huzur (a.t.ba) alisema baadhi ya wanawake wamekuwa wakimwandikia barua kuwa wazazi wao hawataki waolewe na watu wanaowapenda bali hutaka waolewe na watu walio matajiri pasipo ridhaa zao. Akikemea jambo hili Mtukufu Mtume Muhammad (S.A.W) alisema kuwa wanawake wapo huru na hakuna mwenye ruhusa ya kuwashinikiza kwa kuwa haki zao zimekwisha bainishwa. Wanawake wa Kiahmadiyya wanatakiwa wamwamini Mtukufu Mtume Muhammad (S.A.W) na watangulize dini kuliko dunia. Hata hivyo, Huzur (at.b.a) alisisitiza kuwa wavulana wawaoe wanawake ambao ni Waahmadia. Amesema kuwa jambo kubwa hapa ni kuzingatia kigezo cha dini. Aidha, amesema tunapata matatizo mengi kwa ajili ya kutozingatia jambo hili. "Allah Asaidie na huwa ninamwomba sana Atusaidie", alisema. Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alisema wazazi wabinafsi na wanaojali maslahi yao huzikataa posa za mabinti zao na kwa kufanya hivyo wajue kwamba hawaitendei haki Islam.

Akizungumzia kuhusu hijabu, Huzur (a.t.b.a) alisema kuwa mara kadhaa msisitizo umewekwa katika jambo hili. Wengine huhoji kuwa vazi hili linamaana gani katika ulimwengu wa kisasa! Huzur (a.t.b.a) alisema haya ni maagizo ya Kurani Tukufu na kwamba mwanamke wa kweli wa Kiahmadiyya hawezi kuhoji jambo hili. Alisema kuwa hizi ni zama za giza na kwamba amri za Allah haziheshimiwi na zimeachwa. Hijabu haina maana kuwa mwanamke amefanywa mfungwa hivyo wanawake wasijione kuwa wamedhalilishwa bali Islam imewajali. Allah Atusaidie.

Masjid Nasir Yang'ara Mbeya Mjini

(Mwandishi wetu Mbeya)

Kwa fadhili za Mwenyezi Mungu Jumuiya ya Waislam wa Ahmadiyya kwa mara nyingine tena imefungua msikiti mkubwa katika jiji la Mbeya, manispaa ya Mbeya mjini. Ni msikiti wa aina yake mzuri na wa kisasa kabisa. Kwa hakika unavuatia sana. Kijografia na kijamii Mbeya iko nyanda za juu kusini mwa Tanzania, kiasi cha kilometa 828 kutoka Dar es Salaam, kimkoa ina eneo la kilometa za mraba 62,420 na wilaya ya Mbeya mjini yenyewe ina eneo la kilometa za mraba 222. Kwa takwimu za mwaka 2012 Mbeya ina watu zaidi ya Mil 2.7. Wenyeji wa mkoa wa Mbeya ni Wasafwa na Wanyakyusa, ambao shughuli zao kubwa kiuchumi ni kilimo cha viazi, mpunga na matunda kutegemeana na wilaya.

Kiimani asilimia kubwa kabisa ya wenyeji na hata wakaazi wa Mbeya ni Wakristo hasa wa dhehebu la Roman Catholic, ingawa yapo pia madhehebu mengine mengi ya Kikristo mkoani humo. Inasadikiwa kuwa katika mikoa yote ya Tanzania, mkoa huu ndio unaongoza kuwa na makanisa mengi kuliko mkoa mwengine wowote.

Upande wa Waislam wapo ila ni wachache sana, wapo Sunni wachache wakiwa chini ya Bakwata na pia Jumuiya ya Waislam Waahmadiyya iko na matawi yake katika mkoa huu wa Mbeya kama ilivyo katika mikoa mengine hapa nchini.

Historia ya Jumuiya ya Ahmadiyya katika mkoa huu wa Mbeya inaturudisha nyuma kwenye miaka ya 1988/9 ambapo inasemekana kulikuwa na familia chache za Wanajumuiya waliokuwa wakiishi Mbeya, kuna waliohamishwa kikazi na wengine kwa ajili ya maisha tu. Ikiwemo familia ya Dr. Iddy Mwanga, Mzee Ambari Mpulaki, Marehemu Mzee Hassan Thamit Moli na baadae marehemu Zakaria Mchawi. Marehemu Mwalimu Daudi Shoo alifika Mbeya na kuanza kuzifuatilia familia hizi kwa ukaribu zaidi, kwa lengo la kuziunganisha kwa pamoja na kufungua tawi. Ikaamuliwa kuwa wanajumuiya hao watakuwa wakikutana na kufanya ibada nyumbani kwa marehemu mzee Moli eneo la Machinjioni. Inasemekana kwa muda mrefu sana nyumba hiyo ilitumika kwa Wanajumuiya kukutana na kufanya ibada hapo.

Kufikia miaka ya 2005 wazo likaja sasa la kutafuta nyumba maalum ya Jumuiya, Amir na Mbashiri Mkuu wa wakati huo Sheikh Faiz Ahmad (kwa sasa



Masjid Nasir - Mbeya kwenye siku ya ufunguzi

anaishi Uingereza) akaridhia kutafutwe nyumba na Jumuiya itanunua. Alhamdullah nyumba ikapatikana kwa bei nafuu mno eneo la Jakaranda, ambapo inasemekana ilinunuliwa kwa Shilingi za Kitanzania Milioni 5.5 wakati huo. Nyumba hiyo ya Jumuiya ikaanza kutumika kuwa mahali pa uhakika kwa Wanajumuiya kukutana na kufanya ibada na kila kilichohusu Jumuiya, pia ilitumika kama nyumba ya Sheikh wa Mkoa kwa upande mmoja. Baadhi wa walimu na masheikh waliokaa na kufanya kazi za Jamaat Mbeya ni pamoja na Mwl. Daudi Ali Shoo, (marehemu) Mwl Yusuf Mbawala, Mwl. Alli Rashid Kivinga, Mwl. Laban-dinn Amani Lukalango, (marehemu) Mwl. Sadiki Musa Mbawala, Mwl. Makarani Hamza Balama, Mwl. Bashiru Hassan Mrope, Mwl. Shaban Ramadhan, Mwl. Chande Nyenje Komakoma. Masheikh ni pamoja na Sheikh Issa Kanyeka (marehemu) Sheikh Farid Ahmad Tabassam, Sheikh Mubarak Ahmad (marehemu), Sheikh Khawaja Muzaffar Ahmad, Sheikh Bashrat Rehman, Sheikh Karimuddin Shams aliyepo mpaka sasa.

Inasemekana kuwa ni katika kipindi hiki cha Sheikh Karimuddin Shams kwa maana ya kiasi cha miaka miwili iliyopita ndio wazo la kuamua kujenga msikiti kamili na nyumba ya mbashiri lilikuja. Kwa fadhili za Allah juhudi zilifanyika kutoka kila upande na hasa kutoka Markazi ili kufanikisha ujenzi huu. Ndipo mnamo tarehe 28/11/15 saa 7:20 Adhuhuri, Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Waislam Waahmadiyya Tanzania Sheikh Tahir Mahmood Choudhry kwa pamoja na Mkuu wa Wilaya ya Mbozi Mheshimiwa Ahmad Namoye (niaba ya mkuu wa mkoa wa mbeya), walifungua Rasmi Msikiti huu wa kwanza kabisa katika mkoa wa Mbeya, uliopo eneo la Nonde. Jina la msikiti huo ni "MASJID NASIR" Alhamdulillah Thumma Alhamdulillah.

Sherehe za ufunguzi wa msikiti huo ziliandamana na shamra shamra mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuandaliwa kwa Kombe la Ahmadiyya la mpira wa miguu na kualikwa wageni mbalimbali kutoka madhehebu ya dini, viongozi wa serikali nk. Kwa hakika ilikuwa ni tamasha la aina yake. Sherehe za ufunguzi wa msikiti huo zilizofanyika katika eneo la msikiti, zilianza kwa usomaji wa Quran Tukufu iliyosomwa na Mwalimu Ramadhan Shaban na kufuatiwa na shairi lililosomwa na Mwalimu Makarani Hamza.

Kisha ilifuatiwa na nasaha zilizotolewa na Sadri Khuddamul Ahmadiyya Tanzania Twaha Nyange Sahib ambae alitoa historia ya Jumuiya kwa ufupi na kueleza mafaniko makubwa ya Jumuiya ikiwa ni pamoja na kutafsiri Quran Tukufu katika lugha mbalimbali duniani na ujenzi wa misikiti katika kila pembe ya dunia.

Akitoa salamu zake katika hafla hiyo, mkuu wa wilaya ya Mbeya mjini Mh. Nyarembe D. Munasa aliishukuru sana Jumuiya kwa kujenga msikiti wa kisasa mjini Mbeya na kuwa hiyo ni heshima kwa wakazi wa mji huo. Alisema dini ya Islam inasisitiza sana juu ya swala la amani na kuwa kama binadamu tunatakiwa kuwa makini katika kujenga historia nzuri ya maisha yetu ya kidunia ili kuwa na maisha mazuri ya baadae. Alisema Jumuiya ya Ahmadiyya ina jukumu kubwa la kufundisha jamii juu ya maana halisi ya jihadi hasa ya jihadi ya nafsi ambayo ndio ngumu zaidi na kuachana na imani potofu za jihadi ikiwemo jihadi za kivita ambazo ni jihadi dhaifu kabisa. Akisoma hotuba yake iliyojaa nukuu za aina mbalimbali kutoka kwa wasomi, viongozi wa dini na siasa, wanafalsafa nk, mkuu huyo wa wilaya alimnukuu, Baraka Obama; "Audacity of Hope the Dream of my Father", kwa kusema tuendeleze ndoto za baba na babu zetu wa imani kama Hazrat Mirza Ghulam Ahmad mwanzilishi mtukufu wa Jumuiya ya Waislam wa Ahmadiyya.

Akinukuu kutoka kitabu cha Maadili ya Taifa na Hatma ya Tanzania Enzi za Mwalimu Nyerere cha Ibrahim Kaduma, mkuu huyo wa wilaya alisema tuisaidie serikali ya awamu ya 5 kujenga maadili ya taifa yaliyojengwa juu ya neno la Mungu. Tumuombe Mwenyezi Mungu kwa uadilifu ili kupata kiongozi mwadilifu na hajaruhusu viongozi waovu na mafisadi kutawala nchi hii na kubomoa amani tuliyonayo. Mwenyezi Mungu anawapenda na kuwatetea maskini na wanyonge"

Alitoa wito kwa jamii kuitumia vizuri Jumuiya ya Waislam Waahmadiyya inayotumia kila nafasi na fursa zote katika kuhakikisha kuwa usawa, uadilifu, na haki vinatendeka na kustawi na wanadamu wote, popote pale walipo wanapata na kufurahia maisha ya amani na usalama.

Akiongea kwa niaba ya mkuu wa mkoa wa Mbeya, mkuu wa wilaya ya Mbeya Mh. Ahmed Namoye alisema kuwa yeye binafsi amefarijika mno na ujenzi huo katika mji wa Mbeya na kuwa msikiti huo umekuwa nuru mpya katika mji wa Mbeya. Alisema kuwa msikiti huo ni kielelezo kikubwa cha kuonyesha kuwa Jumuiya ya Waislam Waahmadiyya inatenda na sio kusema tu. Alisema tatizo moja kubwa la Waislam wengi ni kuongea sana kuliko kufanya kazi, alisisitiza kuwa hakuna kudi kubalidika na kuacha kusema sana bali watu wajitume zaidi katika kutenda kuliko kusema. Akitoa sifa zaidi juu ya ujenzi wa msikiti huo, alisema kuwa ni vizuri sana kwa watu kujiwekea malengo makubwa zaidi badala ya kuweka malengo madogo na kushindwa kuyatekeleza. Alisisitiza sana swala la utoaji wa elimu na akaomba uongozi wa Jumuiya kufanya mipango thabiti ya kuwa na vipindi vya kutoa elimu msikitini hapo ili kuwawezesha watoto na hata watu wazima kuweza kupata elimu nzuri ya kidini na dunia na kuwa hata kama sisi tukiondoka tuna yakini kuwa wapo nyuma yetu wenye elimu ya kuendeleza yale tuliyoyaacha sisi. Aliitaka jamii kuondoa tofauti zao na kuwa kama kuna jambo zuri limefanywa basi hatuna budi kushukuru na kulitumia jambo hilo vizuri ili liwe kwa manufaa yaliyokusudiwa, bila kujali nani amelifanya au kutenda.

Akitoa salamu katika uzinduzi huo, Sheikh wa Bakwata wa Mkoa wa Mbeya Mohammed Ali kwa niaba ya Bakwata aliipongeza Jumuiya ya Ahmadiyya kwa kuonyesha juhudi kwa vitendo kwa kujenga msikiti huo mzuri na wa kisasa badala ya kuongea sana na kutenda kidogo. Ameishukuru Jumuiya ya Ahmadiyya na kusema yeye binafsi anaifuatilia Jumuiya ya Ahmadiyya kwa ukaribu sana hususan katika kusoma vitabu na vipeperushi vya Jumuiya.

Nae mchungaji wa kanisa la Baptist Kyela ndugu Ambokile Kamendu akitoa salamu kwa niaba ya Kanisa lake alisema ameshangaa mno kwani katika maisha yake hajawahi hata siku moja kukaribishwa katika hafla za Kiislam na kuwa hilo limekuwa ni jambo la ajabu mno kwake, amepata faraja kubwa sana kwa mwaliko huko na hivyo amefanya kila juhudi kuhakikisha anafika. Ameishukuru sana jumuiya kwa mwaliko huo na kusema kuwa Jumuiya imeonyesha kwa vitendo hasa dhana nzima ya "mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote" Akasema kuwa yeye anaamini juu ya Mungu mmoja na kuwa madhehebu yanaweza kuwa mengi lakini msingi ni kuwa madhehebu hufuata dini na si dini hufuata madhehebu, hivyo Mungu na dini inakuwa moja madhehebu hufuata dini ya Mungu mmoja. Katika kuonyesha msimamo na furaha yake, baada ya chakula aliamua kujiunga na wanajumuiya katika swala ya Adhuhuri na

Endelea uk. 9

Sheikh wa Bakwata Mbeya asema:
"Waislamu acheni Fitina, Majungu na fanyeni Kazi"

Mwandishi wetu (Mbeya)

Waislam wameaswa kuachana na fitna, unafiki na majungu na badala yake wajikite katika kufanya kazi na kutafuta maendeleo ya kweli. Kauli hiyo imetolewa na sheikh wa Bakwata wa mkoa wa Mbeya, Sheikh Mohamed Bin Ali alipokuwa akitoa nasaha zake katika ufunguzi wa msikiti wa mkubwa wa mkoa wa Jumuiya ya Waislam Waahmadiyya Mbeya mjini.

Akiongea kwa ufasaha na kwa kujiamini sana, huku akiweka na mzaha kidogo, Sheikh Ali alisema kuwa ni aibu kwa waislam kuendelea kulalamika tu bila kuwa na mipango thabiti ya kujiletea maendeleo, alisema kuwa sehemu kubwa ya waislam wamejikalia tu, hawataki kufanya kazi, wao ni watu wa kukaa maskani kujadili majungu, fitna na kulaumiana.

Kwa upande wa elimu sheikh Ali alisema yeye anapenda sana kusoma na kwa hakika amesema amesoma vitabu vingi vya Jumuiya ya Ahmadiyya na ikiwa ni pamoja na vipeperushi vingi vilivyochapishwa na Jumuiya ya Ahmadiyya na bado anaendelea kusoma kwa nia ya kuufahamu vizuri Uahmadiyya wenyewe lakini pia kujifunza zaidi. Alisema swala la elimu ni swala kubwa na la msingi sana, akitoa mfano kuhusu umuhimu wa elimu, alisema inasikitisha kuwa waislam wana chuo kikuu kimoja tu cha Morogoro ambacho amesema nacho si kwamba kimejengwa na wasilamu bali ni majengo ya Tanesco ndio waislam wamepewa na tangu wapewe hakuna jipya lolote waliloweza kufanya, zaidi ya fitna na majungu miongoni mwa waislam wenyewe. Akasema hii inasikitisha sana, waislam kuishia kukaa vijiweni na kulaumiana tu.

"Wengi hawataki kabisa kujisomea vitabu na kujiongezea elimu na ufahamu wa dini au madhehebu yao, ukizungumzia vitabu vya nje ya madhehebu yao ndio hata kuvigusa hawataki bali wao wameshikilia imani yao tu na hata ukiwauliza juu ya imani yao au imamu wanaemfuata hawajui, ni wavivu wa kila kitu, alisisitiza Sheikh huyo wa Mkoa. Na kusema kuwa hili si jambo zuri kabisa katika jamii ya Kiislam.

Alisema lazima Waislam wabadilike sasa na waige mfano wa Waahmadiyya, kuwa wanasema machache na kufanya mengi. Ametolea mfano kuwa Waislam walio wengi, nguvu yao kubwa ni kulaumu lakini ushiriki wao wenyewe haupo, hawachangii wala hawajishughulishi na lolote zaidi ya kukaa na kulaumu, akasema ni bora basi wangekuwa wanajishughulisha kwa kuchangia au kutoa mawazo kisha ndio wakae pembeni kulaumu lakini hawana mchango wowote si wa hali wala mali bali mchango wao mkubwa ni lawama tu.

Alisema baadhi ya Waislam, ukiwauliza michango au kuchangia jambo huwa wakali au hawapendi, lakini aliwataka wajue kuwa ni kupitia juhudi hizo ndio mambo yanaweza kwenda mbele. Akasema kama wanaogopa sana michango wajiunge na Ahmadiyya kwani huku hakuna michango.

Aliendelea kusema kuwa kwa kuthamini mwaliko wa kuja kwenye ufunguzi wa msikiti huu wa Ahmadiyya mjini Mbeya, Sheikh Mohammed Ali alisema kuwa alikuwa nje ya mji wa Mbeya kikazi na hata kanzu yake nzuri aliivaa akiwa kwenye gari lakini hakuwa radhi kuacha kuhudhuria katika hafla hiyo adhimu ya ufunguzi wa msikiti huo wa Jumuiya ya Waislam Waahmadiyya unaotambulika kama "Masid Nasir" uliopo Mbeya mjini.

Alisema kuwa baadhi ya watu walimkebehi kwa yeye kuonyesha juhudi za kuwahi kwenye hafla hiyo, kuwa kwa nini sheikh unawahi kwenye uzinduzi wa msikiti wa Ahmadiyya, kana kwamba si jambo la muhimu, lakini yeye anasema aliwajibu kuwa, hawajui umuhimu wake ndio maana wanasema hivyo, na kama wangejua basi hata wao wangefanya juhudi za kuwahi.

Akitoa sifa juu ya msikiti huo, sheikh huyo wa Bakwata mkoani Mbeya Mohammed Ali, alisema kuwa uzuri wa msikiti huo mkubwa na wa kisasa unavutia, sio kwa nje tu bali hata kwa muumini kujihisi kuingia na kufanya ibada. Alisema Uislam sio umasikini na kuwa na nyumba za ibada zisizoeleweka au mbaya, alisema kuwa na sehemu nzuri ya kufanyia Ibada inamfanya muumini kuamini na kujithaminisha pia kwa Mungu wake. Msikiti ukiwa mzuri, kama huu wa Jumuiya ya Waislma Waahmadiyya hapa Mbeya unakupa raha na yakini ya thamani ya dua yako kwa Mungu unaemuabudu. Alisisitiza kiongozi huyo wa Bakwata.

Alimalizia kwa kuwataka Waislam waache kukaa vijiweni, kujenga, fitna na majungu na badala yake, wajishughulishe kutafuta vipato vya halali na kubwa zaidi elimu wasome vitabu na wawe tayari kujifunza juu ya madhehebu mingine badala ya kuamini kwa kusikia tu bila kufanya juhudi zao mwenyewe za kujisomea na kuongeza ufahamu wa dini au dhehebu lako na dini au madhehebu mengine pia kwani elimu ni uwanja mpana sana.

Maisha Yangu katika Utumishi wa Jamaat Afrika Mashariki

Kutoka uk. 12

mrefu na Waahmadiyya, lakini hatuna ugomvi na Sheikh huyu Inayatullah na katika kila tatizo anatusaidia, kwa hivyo hakuna haja ya kwenda kushitaki kwa DC.

Nakwanjiahiijambohililikaisha na Jamaat ya RUNGUYA ikaendelea kustawi. Karibu na SIKONGE barabarani kulikuwa na msikiti ulikuwa hausaliwi isipokuwa mwezi wa Ramadhani tu, Mwanajamaat mmoja mpya alishiriki sana katika ujenzi huo nae alikuwa anakaa karibu na msikiti huo, kutokana na ushauri wangu tukausafisha msikiti na Ijumaa moja tukasalia humo mimi, Mwl. Ismail na Mwl. Rashidi Swalehe, baadae tukapata habari kuwa wapinzani waliamua kuuchoma moto. Na kwa ajili hii siku moja walikuwa wanafanya mkutano hapo hapo Sikonge kuhusiana na msikiti huo. Nilipopata habari tu na mimi nikaenda ili niwaambie kuwa Msikiti hauna kosa lolote kama mnataka kuuchoma basi nichomeni mimi. Tulipofika huko Sikonge tukakuta watu wamekusanyika na wamekaa kwenye mstari na Al-Haji Chifu Abdallah Saidi Fundikira alikuwepo hapo amekaa kwenye kiti alipotuona tunakuja yeye akaniashiria nikae kwenye kiti pamoja nae. Wakati huo mpinzani mmoja akasimama na kusema kuwa watu hawa wanakuja kutupoteza na akasema kuwa afadhali Wakristo kuliko hawa. Mimi nilipotaka kujibu Chifu Fundikira sahib akasema kuwa endelea kukaa mimi mwenyewe nitamjibu. Iwe wazi kuwa Mheshimiwa Chifu alikuwa mwanafunzi wa Sheikh Mubarak Ahmad na alikuwa ni rafiki yangu yeye akawaambia watu waliohudhuria pale kuwa misikiti yenu mwaka mzima huwa inakaa tupu ambamo wadudu na panya huzaliana humo. Waislam Waahmadiyya ni ndugu zetu na kwa sauti kubwa akasema wafungulieni msikiti wao watauweka safi na kusalia humo, na yule aliyesema kwamba Wakristo ni bora kuliko Waahmadiyya alikuwa ni Mwalimu wa Shule ya msingi akamgeukia na kumwambia kuwa mimi sipendi mwanangu awe Mkristo mara elfu nitapenda awe Muislam wa Kiahmadiyya. Katika hali hii mambo yakaenda vizuri kwa amani na msikiti haukuchomwa moto.

Na kabla ya hapo wakati wa siku ya maulidi iliyoandaliwa na wasuni Chifu aliwahi kuisikiliza hotuba yangu katika hafla hiyo na aliathirika sana. Na vile vile aliwahi kuona jambo la ajabu kuwa siku moja katika barabara ya NZEGA Tabora kwa kukosa usafiri mimi na Mwalimu Rashidi Swalehe tulikuwa tunaelekea Tabora kwa miguu tukiwa njiani mvua kubwa ikaanza kunyesha kwa wingi kando kando na ilikuwa porini kwenye miinuko ya milima. Tulipokuwa tunateremka mimi ninageuka nyuma na nikaona gari moja Mercedes Benzi lilikuwa linakuja kwa mwendo wa kasi, gari lilikuwa linabendera ya Tanzania ndani ya gari alikuwa Alhaji Fundikira na washauri wake wawili watatu na yeye mwenyewe alikuwa anaendesha, alipotuona akasimama na kuniambia nikae nae mbele na Mwalimu akamwambia akae n yuma na wasaidizi wake sasa mvua iliyokuwa inanyesha kandokando baada ya sisi kuingia ndani ya gari ikaanza kunyesha kwa nguvu sisi kwa kuona fadhili za Mwenyezi Mungu zimetusaidia na kutuokoa katika janga tukafanya maombi sana na kumshukuru Allah Alhamdulillah Rabbil'alamin.

Mambo mengi siwezi kuyakumbuka lakini kwa uchache kwamba safari moja balozi wa India alitutembelea Tabora Msikitini kwetu, vilevile bwana Sayyid Muhammad Afzal sahib aliyekuwa balozi wa Pakistan Afrika Mashariki pia aliwahi kututembelea tukawakirimu na tukawapa vitabu na majarida ya Jamaat. Vivyo hivyo baada ya kupata kibali cha maandishi tulikuwa tunawatembelea wafungwa magerezani na wanajeshi na wagonjwa hospitalini.

Marehemu Sheikh Amri Abedi Kaluta kama nilivyoeleza hapo juu tulikuwa na upendo wa dhati kabisa baina yetu mwaka 1960 nilipopelekwa Uganda kwa mwaka mmoja marehemu Sheikh Amri Abedi akamwambia Amir na Mbashiri Mkuu wa Afrika Mashariki (Maulana Sheikh Mubarak Ahmad) kuwa kwa nini unampeleka Mbashiri wetu Uganda kutoka Tanzania?

Lingine ni kwamba ni mimi ndiye niliyefungisha ndoa yake ya pili baina yake marehemu Sheikh Kaluta na Bi. Amina Hamisi Mlenzi, na ni mimi ndiye niliyeongoza sala ya jeneza ya marehemu Sheikh Kaluta Amri Abedi mjini Dar es Salaam baada ya kufariki kwake.

Alhamdulillahi A'laa Dhaalika.

Sifa zote njema zinamhusu Allah juu ya haya yote.

Wassalaam

Mhitaji wa maombi mtumishi hakiri

Choudry Inayatullah Ahmad
Amir mstaafu wa Jamaat ya Tanzania na Kaimu wa Raisultabligh wa Afrika Mashariki.

Masjid Nasir Yang'ara Mbeya

Kutoka uk. 8

Alasiri zilizoongozwa na Amir na Mbashiri mkuu.

Naye Amir na Mbashiri mkuu katika salamu zake wakati wa ufunguzi wa msikiti huo, alisema kuwa, kufunguliwa msitiki ni jambo moja lakini kuutendea haki ni jambo la pili kwa maana ya kuhakikisha kuwa lengo au dhumuni la kujengwa nyumba hiyo ya ibada linatimia. Alisema ni muhimu kwa kila Mwanajumuiya kuhakikisha kuwa anapata muda wa kufika msikitini na kufanya ibada zake hapo hasa za jamaa. Alisema anafahamu kuwa wapo wanaoishi mbali kidogo na msikitini lakini akasema ni lazima watu kufanya juhudi ya makusudi kuhudhuria msikitini kama si kwa swala zote tano basi japo tatu kwa siku wahakikishe kuwa wanaswali msikitini.

Akisisitiza hoja yake hiyo sheikh Tahir Mahmood Chaudhry, Amir na Mbashiri mkuu wa Jumuiya ya Waislam Waahmadiyya Tanzania alinukuu Quran Tukufu "Na kwa hakika misikiti yote ni ya Mwenyezi Mungu basi msimuombe mwengine pamoja na Mwenyezi Mungu (72;19)" hivyo kusisitiza watu wafike msikitini kufanya ibada, ili kutumiza haki hiyo ya nyumba ya Mwenyezi Mungu, alisema lengo kuu la kuumbwa binadamu ni kumuabudu Mwenyezi Mungu na akanukuu aya nyengine ya Quran tukufu "Sikuwaumba majini na watu ila wapate kuniabudu" (51;57) Sheikh Sahib akasisitiza kuwa binadamu hana budi kufanya juhudi kuwa karibu na Mwenyezi Mungu kwani kwa kufanya hivyo ndio kunatimiza lengo la kuumbwa kwake na msikiti kama nyumba ya Mwenyezi Mungu ni sehemu nzuri ya kufanya juhudi hizo. Sheikh aliongoza maombi ya kimya na kukamilisha shughuli hiyo.

Maisha Yangu katika Utumishi wa Jamaat Afrika Mashariki

Kutoka uk. 12

na kuwahutubia vijana waliokuwa wamejaa chumbani hapo na kwa kumuona mgeni (mimi) wanafunzi wa Kikristo pia walikuja kunisikiliza. Wanafunzi wawili Waahmadiyya pia walikuwepo yaani Mheshimiwa Sheikh Amri Abedi Kaluta na Mheshimiwa ndugu Jumanne Abdallah sahib. Baada ya kupata uhuru wa Tanzania miongoni mwao walipata nyadhifa kubwa akiwemo mwanafunzi Bw. Julius Nyerere nae pia alikuwa amehudhuria. Na kwa njia hii mwaka 1940 na 1941 mimi nikapata fursa ya kuitumikia nchi ya Tanzania kwa njia ya kujitolea. Alhamdulillah. Mwaka 1943 nilipokuwa nimeajiriwa jeshini, nilipata likizo na nikiwa nimefikia katika nyumba ya Mheshimiwa Sayyid Mahmudullah Shah sahib, nikaandika barua kwa Hadhrat Muslih Mauud (ra) ya kujitolea wakfu niitumikie dini na kwa fadhili za Allah akanikubali na akasema kuwa baada ya kuacha kazi jeshini nikakaa mwaka mmoja na Maulana Sheikh Mubarak Ahmad. Ndivyo ilivyokuwa kwamba mara tu nilipoacha kazi jeshini nikaenda Nairobi kuanza kufanya kazi za dini. Nilikuwa nimefanya kazi pembezoni mwa Nairobi kwa miezi michache tu pale Sheikh Amri Abedi sahib aliyekuwa amepangiwa kufanya kazi maeneo ya Kisumu Kenya alipomwandikia barua Hadhrat Muslih Mauud (ra) kuwa mimi siwezi kufanya kazi peke yangu, afadhali aletwe Sheikh mmoja wa Kipanjabi aje afanye kazi hapo. Mimi nikapata simu yenye maagizo ya kwenda huko. Na mimi Novemba 1946 nikaenda tukakabidhiana uongozi huko Murumba. Kijiji hiki kikpo umbali wa maili 35 kutoka mjini Kisumu kwenye barabara inayoelekea Uganda. Baada ya kukaa na mimi miezi michache Sheikh Amri Abedi sahib akarejea Tanganyika. Mimi nikabakia na Mwanajamaat mmoja mwafrika Bw. Fazal Ahmad Odera tukawa tunaendeleza mahubiri katika eneo hili la rizavu kwa ajili ya waafrika. Kwa kufanya kazi pamoja na Sheikh Amri Abedi sahib kwa mara ingine tena tukaendeleza mahusiano yetu na Tanganyika.

Tarehe 02 Disemba mwaka 1947 Maulana Sheikh Mubarak Ahmad akafungisha ndoa yangu mjini Tabora na bi. Iftikhar Begum binti wa Sheikh Mubarak Ali Sultan Bakhsh sahib wa Isaka. Mke wangu alizaliwa tarehe 12/06/1930 mjini Kahama na kwa njia hii mahusiano na Tanganyika yakazidi kuimarika.

Mwaka 1951 baada ya kurejea Afrika Mashariki kutokea mapumzikoni ya likizo Pakistan nikiwa bado niko Mombasa nikapata maagizo ya kwenda moja kwa moja Tabora nikachukue usimamizi wa kituo hicho pamoja na kiwanda kidogo cha uchapishaji kilichokuwepo pale.

Mwaka 1949 Raisultabligh wetu Maulana Sheikh Mubarak Ahmad alipokwenda likizo nchini Pakistan Hadhrat Amirul Mu'uminin Khalifatul Masih –II (ra) akaniteua mimi kukaimu nafasi ya Mubashiri Mkuu na Amir Jamaat wa Jamaat za Afrika Mashariki. Katika kutekeleza majukumu yangu ikabidi nifanye safari ndefu nchini Tanganyika.

Mwaka 1956 kwa mara ya pili Maulana Sheikh Mubarak Raisul tabligh akaenda tena likizo Pakistan, na kwa mara hii tena Hadhrat Khalifatul Masih wa pili (ra) akaniteua kukaimu nafasi hiyo. Wakati huo nikafanya ziara ya Tanganyika nzima. Kutokea Lindi mpaka Songea n.k. nikatembelea Bukoba, Mwanza, Kigoma na Tanga. Mwaka 1960 Sheikh Abdulrahman Misri alifika Uganda kueneza sumu yake, kwa ajili ya kuiondoa sumu hiyo, Raisultabligh akanipeleka Uganda nikakaa kule miezi sita kwanza na baadae nikakaa miezi mitano mingine na kwa fadhili za Allah Jamaat za Uganda zikaepushwa na fitina za Sheikh Misrii. Yeye akarejea kwao bila mafanikio yoyote huku ameshindwa vibaya.

Mwaka 1956 nikatembelea maili kumi na mbili kutoka Lindi mjini walipokuwa wameweka kambi Wanajamaat na kuzalisha mzozo ambao baada ya mimi kufika huko tukaumaliza mzozo huo. Baada ya suluhu kufanyika Wanajamaat wote wakashikana mikono kwa furaha na uchaguzi wa viongozi ukafanyika. Kwa vile eneo hilo halikuwa na jina, hivyo rai ikapelekwa kwa Khalifa Mtukufu kuwa eneo hili la Wanajamaat liitwe Qadian. Hazur akarudisha jibu kuwa jina hili ni zuri, sana na kwa hali hii ya ruhusa ya Khalifatul Masih (ra) jina la Jamaat hii likawa Qadian wilaya ya Lindi.

Mwaka 1954 rafiki mmoja mpakistani msuni, pamoja na Bw. Muhammad Afzal Khan na mbele ya Waziri Muhammad wakaniuliza kama naweza kuomba dua ya upande mmoja yenye kiapo cha maangamizi kama alivyoomba Hadhrat Muslih Mauud (ra). Kutokana na msisitizo wao nikaomba kuwa kama Hadhrat Masihi Mauud (as) alikuwa muongo na kwamba mimi ninafanya kazi yake yenye uongo, basi Ee Mola niangamize katika muda wa mwaka mmoja na uwafurahishe maadui wa Jamaat Ahmadiyya. Dua hii niliiomba mwaka 1954 lakini mpaka leo 1992 mimi niko hai na ninaendelea kuwaita watu kwenye muongozo wa haki. Baada ya maombi haya Muhammad Kalufya wa Uvinza akajiunga na Jamaat na baada ya kujaza Baiat watu wa kabila lake wakamchagua yeye awe chifu wao. Baadae alipata upinzani mkali sana. Lakini mara zote Allah Alimuepusha na kila shari. Alhamdulillah. Chifu Muhammad ni chifu wa kwanza Muahmadiyya na watoto wake ni Waahmadiyya waaminifu sana.

Baada ya maombi haya ya upande mmoja nikafanya mjadala na mapadri wawili waliotoka Afrika Kusini katika Kanisa la Katoliki mjini Tabora. Wao walikuwa wamedai kuwa hakuna dalili ya ukweli wowote wa Mtume Muhammad (saw) ndani ya Biblia. Sisi tukachapisha vipeperushi elfu kumi na tano kuthibitisha juu ya ukweli wa Mtume Muhammad (saw) na kukanusha juu ya uungu wa nabii Isa (Yesu Kristo). Tukawataka tufanye nao majadiliano popote watakapo. Lakini wakatishika na ukweli nao wakakimbia bila hata kuaga. Baada ya hapo m imi nikafanya safari ndefu ya Tanganyika. Nikaenda Shinyanga, Mwadui, Mwanza, Bukoba, Kigoma, Sumbawanga, Mpanda, Kirando, Uvinza, Malampaka, Ifakara n.k huko tukawaita mapadri kwenye mashindano, lakini hakuna yeyote aliyejitokeza.

Mwaka 1957 kwa TANU kupewa madaraka wakafanya sherehe kubwa kwa kusherehekea mafanikio hayo na mikutano mbalimbali ikafanyika ambapo kati ya wasio waafrika ni mimi tu ndiye niliyepewa fursa ya kuhutubia hadhara hii. Mwezi Machi mwaka 1960 pale Mwl. J. K. Nyerere baada ya nchi kupata madaraka alizuru Tabora, m imi nniliteuliwa kumtolea risala ya ukaribisho minghairi yangu hakuna mwingine aliyeruhusiwa kumsomea risala yoyote ile, nikamkabidhi vitabu vya Jamaat pia. Mwaka 1970 nilikwenda Ifakara na kutoa hotuba kwa Kiingereza katika Kwiro Secondary School juu ya mada ya uwepo wa dhati ya Allah kwa dakika arobaini na nusu saa ilitumika kujibu maswali ya wanafunzi juu ya ufafanuzi wa mada niliyotoa. Shule hii iko huko Mahenge na inamilikiwa na Kanisa Katoliki. Mwaka 1958 Chifu Secretary wa Serikali ya Kenya Sir Evelin Baring alipoteuliwa Gavana na kuletwa Tanganyika nae akaalikwa na umma kwenye hafla moja huko Nairobi, katika hafla hiyo mheshimiwa akaelezwa mambo yanayohusu kazi za Jamaat na akaathirika sana na akasema kuwa mimi daima huathirika sana na Waahmadiyyana akaniuliza kuwa ninyi huwa mnasomea wapi?

1961 Provincial Commissioner wa Mwanza Bw. Bell alifanyiwa tafrija ya kuagwa na chama cha wafanya biashara (Chambers of Commerce), tafrija hiyo ilifanyika mjini Musoma na mimi niliombwa nitoe hotuba katika hafla hiyo. Hotuba hiyo ilimuathiri sana mgeni rasmi na wahudhuriaji pia.

Mwaka 1963 wakati wa Jalsa Salana yetu iliyofanyika m jini Tabora Mheshimiwa Chifu Abdullah Fundikira Waziri wa Sheria alimualika Alhaji Ahmad Okashi wa Arusha nyumbani kwake kwa chakula, katika kujibu swali nililomuuliza kuwa kama asilimia kumi ya wananchi wa Tanzania wajiunge na Jamaat Ahmadiyya je Waislam wanaweza kuendelea kudhulumiwa? Yeye akakiri mbele ya wageni wote kuwa haiwezekani.

Mwaka 1962 mimi nikifuatana na Mwl. Omar Abdullah tulifanya safari ya Iringa tulikokaa siku tatu nne hivi na kwa fadhili za Allah watu 26 wakajaza Baiat na kujiunga na Jamaat baada ya hapo uchaguzi ukafanyika na tawi la Jamaat likawa limeanzishwa rasmi Alhamdulillah.
Mwaka 1961 uchaguzi wa wabunge ulipoanza kufanyika, viongozi wa TANU wakanitaka nichukue fomu ili nami nigombee nafasi ya ubunge. Siku zile utaratibu ulikuwa hivi kuwa kulikuwa na kura tatu. Moja ya Wazungu, kura moja ya Waasia na kura moja ya Waafrika. Lakini mimi kwa kutopata ruhusa kutoka Makao Makuu sikuchukua fomu ya kugombea nafasi yoyote ile. Kwa vile wapinzani wa Jamaat walikuwa wameweka athari serikalini kuwa ukilinganisha Wahindu na Ismailia wa Agakhani Waahmadiyya hawana umuhimu wowote juu ya hao, hivyo basi mimi kwa kulitanguliza jina la Allah nikaanza kujihusisha na mambo ya kijamii, matokeo yake yakawa hivi kuwa kwa urahisi sana tukafanikiwa kupata kibali cha kuanzisha shule ya msingi ya Jamaat huko Pangale nje kidogo ya mji wa Tabora ambayo hata hivyo, mwaka 1967 baada ya mimi kuondoka kurudi Pakistan shule hiyo ikataifishwa na serikali.

Mwaka 1962 Tabora Chambers of Commerce kwa baraka tu za Jamaat wajumbe wakanichagua mimi kuwa Katibu wake Tabora. Kutokana na mizozo ya wapangaji nyumba mjini Tabora mimi nilitoa rai kwa Naibu Kamishna wa Mkoa afadhali kiundwe chombo cha kurekebisha pango za nyumba, rai hii ikakubaliwa na mimi nikachaguliwa niwe Katibu wa kujitolea kumaliza mizozo na migogoro ya upangishaji nyumba na mara zote mazungumzo yalikuwa yakiongelewa na mashauri yote yalikuwa yakikatwa hapo hapo ofisi ya Msikitini kwetu.

Mwaka 1954 mimi nikateuliwa kuwa Mwenyekiti wa Pakistan association mkoani Tabora.

Mwaka 1955 mimi nikachaguliwa Katibu wa Kamati ya kushughulikia eneo la Makaburi ya Waislam mjini Tabora.

Katika hadhi ya Katibu wa Chambers of Commerce niliandikiana barua na Serikali ya mjini Tabora kuhusiana na uhaba wa maji mjini Tabora. Gavana mwenyewe akaja na akaahidi kutengeneza na kuharakisha ujenzi wa BWAWA LA KAZEMA, na kutokana na ujenzi wa bwawa hilo uhaba wa maji mjini Tabora ukawa umeendoka.

Mwaka 1963 Serikali ya Wilaya ikaniteua kuwa Mjumbe wa Halmashauri ya maendeleo ya Wilaya ya Tabora ambapo msimamizi wa kila kitengo alikuwa ni Mjumbe. Hii ilitoa nafasi nzuri sana ya kufanya mahubiri.

Mwaka 1962 ujumbe wa Tabligh Jamaat kutoka Pakistan tulikutana nao katika msikiti mkuu wa suni, nikawaalika waje msikitini kwetu lakini wakataa na wakakimbia.

Mwaka 1964 wasomaji wa Qur'an kwa kughani walikuja kutoka Msri tukawakaribisha msikitini kwetu wakafika.

Mwaka 1964 kiongozi maarufu wa Kirumi Prof. POTOKHIN alipotembelea Tabora alikuja mpaka msikitini kwetu, nikamhubiri kwa masaa matatu. Aliporejea kwao akaniletea Qur'an moja kubwa kupitia ubalozi wake nchini ambayo iko Tabora au Dar es salaam. Kwanza alikataa kuja lakini akafika msikitini kwetu kimuujiza tu.

Mwaka 1968 nikakabidhiwa uongozi wa mkoa wa Morogoro. Msikiti wa Morogoro na nyumba ya Mbashiri zikajengwa chini ya usimamizi wangu. Tukaandaa banda la maonyesho ya vitabu kwenye maonyesho ya Serikali yaliyofana sana. Watu wakahubiriwa sana.

Mwaka 1956 nilipokuwa nakaimu nafasi ya Raisultabligh wa Afrika Mashariki, mbali na kufanya ziara nchini Uganda na Kenya, mjini Dar es salaam nikaanzisha jarida la Habari za Ahmadiyya kwa Kiswahili ambapo mhariri wake akawa ni Mheshimiwa Sheikh Amri Abedi sahib, kwani gazeti hili hapo kabla lilikuwa likitoka kwa lugha ya Kiurdu tu. Wakati huo nikatembelea Jamaat zote za Tanganyika zikiwemo Kibaha, Madina, Jangwani, Qadian Lindi, Tanga, Moshi, Mtama na Arusha. Mimi nimekaa Tabora kuanzia mwaka 1951 mpaka 1965 yaani jumla ni miaka 14. Katika kijiji cha Runguya hakukuwa na Jamaat. Mimi na Mwl. Rashidi Swalehe tulienda huko na kuwa wageni wa Imam wa Msikiti wa kisuni hapo hapo. Siku hiyo watu wawili watatu wakajaza Baiat na kujiunga na Jamaat. Siku ya pili baada ya sala ya Ijumaa nikatoa hotuba. Baiat zingine nyingi zikapatikana. Waliokuwa wapinzani wakaondoka. Kwa vile Imam wa Msikiti yeye mwenyewe ndiye aliyejengesha msikiti huo jamaa wengi wakajiunga pamoja nae.

Ujumbe wa upinzani ukaenda Tabora wakashtaki kwa Sheikh mkuu Sheikh mzee Fereji, wakasema kuwa Sheikh wa Kiahmadiyya amefanya mahubiri katika msikiti wetu na ameuteka. Mzee Hamisi Mlenzi (Babu yake na Sheikh Bakri) alikuwa anasikiliza maongezi yao akaja kutuambia kuwa Sheikh Fereji kasema hivi; Sisi tulikuwa na ugomvi wa muda

Endelea uk. 9

MKUTANO WA 124 WA MWAKA WA QADIAN:

Kutoka uk. 12

nimeweza kushiriki Jalsa hiyo. Hii inaonesha umoja. Aidha, walioko London wanaweza kufuatilia na kuona tukio linaloendelea Qadian na kwa wakati huo huo walioko Qadiani wanaweza kuwaona wenzao walioko London. Teknolojia hii ambayo ipo katika zama za Masihi Aliyeahidiwa a.s inasaidia kueneza ujumbe wa Islam", alisema Khalifa Mtukufu (a.t.b.a).

Huzur a.t.b.a alisema kuwa jambo hili linathibitisha kwamba Mungu wa Islamu yungali hai. Alisema kuwa baadhi ya bishara zilitimia wakati wa zama za Mtukufu Mtume Muhammad S.A.W, nyingene zilitimia baada ya kifo chake na nyingine zinatimia wakati wa zama za Masihi Aliyeahidiwa a.s.

Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alisema kuwa sambamba na teknolojia hii shetani pia anafanya jitihada ili watu wawe mbali na Mwenyezi Mungu kwani baadhi ya chaneli za televisheni zinaonyesha sinema na picha za aibu. Sisi Waahmadiyya pia tunaishi katika zama hizi za teknolojia ya kisasa, hivyo, tusizitumie zikatufanya tuwe nje ya mwongozo. Tunatakiwa tujaribu kunufaika na teknolojia hizi zinazotuonesha kuwa na umoja. Pamoja na kwamba tu wachache na rasilimali zetu ni finyu, Allah Ametupatia teknolojia hii.

"Pamoja na uzuri wa teknolojia hii, leo hii upo pia uovu na ukatili wa kiwango cha juu unaofanywa duniani. Teknolojia ya kisasa inatumiwa vibaya na watu wengi kwa lengo la kueneza ushawishi wa shetani na uonevu na matokeo yake mtu anakuwa mbali na Mwenyezi Mungu na imani ya kweli. Leo hii ni chaneli ya Kimataifa ya Jumuiya ya Waislamu Ahmadiya pekee (MTA International) inayorusha matangazo ya amani, wema na uchamungu kwa saa 24 kila siku kwa kufuata mafundisho sahihi ya Mwenyezi Mungu na ya Mtukufu Mtume Muhammad S.A.W", alisema.

Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alisema licha ya ufinyu wa rasilimali za Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya, televisheni ya MTA imekuwa ni nyenzo ya kuendeleza muunganiko wa kipekee baina ya Ukhalifa na wanajumuiya kote duniani.

"Makundi mengine yana utajiri mkubwa na rasilimali nyingi lakini bado nchi hizo au viongozi wao wa kidini hawana muunganiko wa moja kwa moja na wafuasi wao duniani kwa kiwango hiki cha Ahmadiyya. Neema hii pekee imepewa kwa Jamaat iliyoanzishwa na Masihi Aliyeahidiwa a.s.", alisisitiza Khalifa Mtukufu (a.t.b.a).

Mtukufu Mtume Muhammad S.A.W alitabiri kuwa wakati wa Masihi Aliyeahidiwa a.s ujumbe wake utasambaa duniani kote. Huzur (a.t.b.a) alisema kuwa wenye bahati ni wale waliopo katika zama hizi na wanafaidika na teknolojia hii. Kila Muahmadiyya aliyeko katika pembe ya dunia anasikiliza sauti ya Khalifa. Ni kwa namna ilioje Mola wetu Ametuonesha uthibitisho wa bishara hizi jambo ambalo linatuzidishia imani! Hivyo, tunatakiwa tutekeleze amri zote kwa juhudi.

"Kwa Msaada wa Allah, Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya imeenea duniani kote. Imeenea Magharibi na Mashariki, Kaskazini na Kusini. Imeenea Barani Afrika, Asia, Ulaya, Amerika, Australia na visiwa vyote. Waislamu Waahmadiyya, popote walipo wameungana chini ya bendera moja. Leo hii, sauti ya Khalifa wa zama inasikika pande zote kama alama ya Umoja wa Mwenyezi Mungu na inaeneza ujumbe wa Uislamu wa kweli katika pande zote za dunia", aliongeza.

Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) aliendelea kusema kuwa:

"Wenye bahati hasa ni wale ambao wameketi Qadian, 'nyumbani' kwa Masihi Aliyeahidiwa a.s, wakishiriki pamoja katika mandhari ya kiroho ya Mkutano wa Mwaka huku wakisikiliza maneno ya mtumishi mnyenyekevu, Khalifa wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. Isitoshe, Waislamu Waahmadiyya katika pande zote za dunia wanaangalia moja kwa moja tukio hili. Bila kujali kama ni mchana au usiku, asubuhi au jioni. Waislamu Waahmadiyya duniani kote wameungana wakitazama tukio hili la Qadian wakishiriki na kufaidika kiroho."

Miaka 108 iliyopita watu wachache walikuwepo Qadian ili kueneza ujumbe huu kwa kujitolea sana ambapo Masihi Aliyeahidiwa a.s alitoa ujumbe huu kuwafikia watu wote, na wakati unawadia kuwa mji wa Qadian utafahamika duniani kote, nanyi leo ni mashahidi wa hilo licha ya kuwepo maelfu ya mamula wapinzani.

Wakati wa Mtukufu Mtume Muhammad S.A.W ujumbe wake ulienea haraka sana katika Bara Arab lakini baadaye watu hao wakaachana na mafundisho ya Islam. Sasa ni jukumu la Waarabu kueneza ujumbe wa Ahmadiyya duniani kote.

Mwaka 1907 Waahmadiyya wakiwa wachache kwa idadi, Masihi Aliyeahidiwa a.s alisema kuwa maadui wanafanya jitihada kupinga ujumbe usienee. Leo hii Qadian kuna Waahmadiyya kutoka sehemu mbalimbali ikiwemo Afrika. Mamula wanajaribu kwa kila hali kutupinga, lakini kwa juhudi zozote wanazozifanya wanaishia kushindwa na kudhalilika. Leo hii idadi ya Waahmadiyya imeongezeka, mathalani barani Afrika mamia kwa maelfu wanajiunga na jumuiya hii kila mwaka. Kila siku Ahmadiyya inapata mafanikio.

Aidha, mwaka 1907 Masihi Aliyeahidiwa a.s alisema kuwa hakuna anayeweza kuzuia nguvu ya Allah kuenea kwa ujumbe wa Jumuiya Ahmadiyya. Akifafanua hili katika kitabu chake cha Baraheen Ahmadiyya kuhusiana na idadi ya watu watakaoungana naye, Mwenyezi Mungu Alimwambia kuwa: 'Ingawa kwa sasa uko peke yako, wakati unawadia kuwa hautabaki peke yako, watu watakuja kutoka pande zote kuungana nawe na watu wa duniani kote wataungana nawe. Nitakusaidia, Nitakulinda na Nitakufanya Imamu wa watu'. Huzur (a.t.b.a) alisema kuwa wakati huo walikuwepo watu 700 tu waliojumuika kwenye Jalsa Salana ya Qadian. Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alisema kuwa leo hii katika Jalsa Salana ya Qadian mbali na washiriki kutoka India, kuna wawakilishi kutoka katika nchi 44 wanaoshiriki Jalsa Salana hiyo.

"Kuna wakati ambapo sio tu Masihi Aliyeahidiwa a.s alikuwa hafahamiki bali pia hata kijiji cha Qadian hakikuwa kinafahamika, lakini leo watu kutoka nchi mbalimbali wamekuja kuhudhuria Jalsa ya Qadian. Kwa hakika, kila mmoja aliyeketi hapo Qadian inaashiria dalili ya ukweli wa Masihi Aliyeahidiwa a.s", alisema Khalifa Mtukufu (a.t.b.a).

Hivyo, Huzur (a.t.b.a) alisema leo hii ninyi nyote ni mashahidi wa ukweli wa ahadi za Masihi Aliyeahidiwa a.s ambapo ujumbe wake umeenea katika nchi takribani 207 duniani kote. Ahadi hizi hazikutoka kwa Masihi Aliyeahidiwa a.s bali kwa Mwenyezi Mungu Mwenyewe na zinaendelea kutimia.

Huzur (a.t.b.a) alisema kuwa Allah Alimweleza Masihi Aliyeahidiwa a.s kuwa: 'Nitakufanya Imamu/ kiongozi duniani'. Akifafanua Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alisema kuwa Allah Ameleta Ukhalifa wa Ahmadiyya na hii ni kwa sababu ya kutimiza ahadi alizompatia Masihi Aliyeahidiwa a.s.

Akieleza jinsi Allah Anavyoendelea kujaalia nyoyo safi kujiunga na Imamu wa zama, Huzur (a.t.b.a) alitoa mifano kadhaa ambapo alisema kuwa Mali ni nchi ambayo miaka 90 iliyopita hakuna aliyeifahamu Qadian, lakini mwaka 2012 kituo cha redio Ahmadiyya nchini humo kilianza kueleza kuhusu ujumbe wa Masihi Aliyeahidiwa a.s huku watu wengine wakiona ugumu wa kujiunga na Jamaat Ahmadiyya lakini Allah Aliwajaalia baadhi yao kama Bw. Lasin Sahib ambaye alikuwa akisikiliza Redio Ahmadiyya na wala hakuwahi kufikiria kama siku moja angejiunga na Jamaat Ahmadiyya. Bw. Lasin alipolala usingizi aliona katika ndoto Khalifa akitembea. Alipoamka akagundua kuwa Khalifa wa Ahmadiyya ndiye yuleyule aliyemuona ndotoni na akajiunga na Jumuiya Ahmadiyya. Huzur (a.t.b.a) alisema kuwa Mamula leo hii ni wagumu kubadilisha mila zao na pia ni wapinzani wakubwa wa ujumbe wa Ahmadiyya.

Huko Ufaransa bw. mmoja alikuwa Ahmadiyya lakini mkewe hakuwa Ahmadiyya. Bw. huyo alimuomba Huzur (a.t.b.a) amfanyie maombi mkewe ili ajaaliwe mtoto. Huzur (a.t.b.a) alisema kwa fadhili za Allah mkewe huyo akapata ujauzito na akajaaliwa mtoto wa kiume aliyepewa jina la Bashir-udin, na hatimaye mkewe huyo akajiunga na Jamaat Ahmadiyya.

Aidha, Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) akisimulia tukio lingine alisema kuna mama mmoja ambaye alikuwa ni Ahmadiyya lakini mumewe hakuwahi kuwa hata Muislamu. Mama yule alimuomba Mwenyezi Mungu kuwa ikiwa hii Jamaat ni ya kweli basi mumewe aongozwe ili awe Ahmadiyya. Yule mume akaja kufanya Bai'at na akajiunga na Jamaat Ahmadiyya.

Huzur (a.t.b.a) alisema: "Leo kwa msaada wa Allah takriban nchi 207 zimepata sauti ya ujumbe wa Masihi Aliyeahidiwa a.s kutoka Qadian. Watu hawa wote ni uthibitisho wa maombi yaliyofanywa na Masihi Aliyeahidiwa a.s. Hivyo, hii ni kudra ya Allah na bendera ya Islamu imepeperushwa kote duniani."

Mwishoni, Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alisoma maneno ya Masihi Aliyeahidiwa a.s akiwaonya wapinzani wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya:

"Enyi watu mnaonisikiliza! Mwogopeni Allah. Allah Afungue nyoyo za watu wasiwasikilize mamula wapinzani na badala yake wasikilize ujumbe wa Masihi wa zama."Huzur (a.t.b.a) alimwomba Allah Atuwezeshe kueneza ujumbe huu na watu wajiunge na Jumuiya ya Masihi wa zama.

Akihitimisha, Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alitaja mashambulizi ya kigaidi yaliyofanywa siku chache zilizopita dhidi ya Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya nchini Bangladesh na tukio la hivi karibuni kuhusu Muahmadiyya aliyeuawa shahidi huko Kyrgyzstan. Kufuatia matukio haya, Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) aliwataka Waislamu Waahmadiyya kote duniani kutopuuza na kuchukua tahadhari ipasavyo dhidi ya matishio ya vikundi vyenye msimamo mkali na vya kigaidi. Aidha, alimwomba Allah Awalinde Waahmadiyya kote duniani. Allah Awezeshe washiriki kupata baraka za Jalsa Salana na Awarejeshe majumbani salama salimini. Amin.

Mkutano ulimalizika kwa maombi ya kimya na kufuatiwa na mashairi mbalimbali yaliyoghaniwa na wahudhuriaji waliokuwa Qadian yaliyorushwa kwa njia ya satellite.

Ufunguzi wa Masjid Nasir Mbeya

Mchungaji atinga Msikitini kufanya ibada

Na Jamil Mwanga

Katika kile kinachoonekana kuwa ni kuvutiwa na mafundisho ya dini tukufu ya Islamu, hatimaye Mchungaji Ambilile Kamendu wa Kanisa la Baptist la Kyela aliamua kuingia na kusali katika msikiti wa Ahmadiyya ulioko mjini hapa.

Tukio hilo la kusisimua lilitokea wakati wa hafla ya ufunguzi wa msikiti (Masjid Nasir) wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya uliopo katika eneo la Nonde, mjini Mbeya ambapo Mchungaji Ambilile alikuwa miongoni mwa viongozi kutoka madhehebu ya dini ya kiislamu na kikristo walioalikwa kuhudhuria hafla hiyo.

Wakati wa Sala ya Adhuhuri na Alasiri ulipowadia, ndipo Mchungaji huyo alipoingia msikitini na kupanga safu tayari kwa kuswali. Kwa mujibu wa rais wa Jamaat ya Mbeya, Dk. Iddi Mwanga, Mchungaji huyo ambaye ni mtu mzima kwa umri, alikaribishwa ili aweze kuswali na kuombea Baraka za msikiti sawa na azma yake hiyo njema.

"Kwakuwa hakuzoea kuswali msikitini, tulimpatia kiti akaketi kwenye safu na kuendelea kuomba huku akifuatisha tunavyoswali kwa adabu na utulivu", alisema Dk. Mwanga.

Akionyesha kufurahishwa na mwaliko huo kutoka kwa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya,



Picha ya pamoja baada ya ufunguzi wa Masjid Nasir Mbeya

Mchungaji Ambilile alionekana mwenye furaha muda wote huku akiomba kupiga picha ndani ya msikiti akiwa na Sheikh Tahir Mahmood Chaundry-Amir na Mbashiri Mkuu, Sheikh Karimdin Shams-Mbashiri wa Mkoa wa Mbeya na Dk. Iddi Mwanga, Rais wa Mkoa wa Mbeya.

Msikiti wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya (Masjid Nasir) ulioko mjini Mbeya ambamo Mchungaji Ambilile Kamendu wa Kanisa la Baptist la Kyela aliingia na kufanya ibada.

Aidha, Mchungaji huyo alisifu kitendo cha ufunguzi wa msikiti kuwa ni cha ki-ungu na kutaka kushiriki bega kwa bega katika kila tukio ikiwamo kutoa nasaha, kupata chakula cha pamoja na kama hiyo haitoshi kuswali ndani ya msikiti huo. "kama nimekuja kufungua msikiti, kitendo ambacho ni cha ki-ungu kwanini nami nisiingie msikitini nikaswali na wenzangu?", alihoji mchungaji huyo ambaye hii ni mara yake ya kwanza kupata mwaliko kutoka kwa Waislamu.

Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya yenye kaulimbiu ya "MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE" imekuwa na kawaida ya kushirikiana na viongozi mbalimbali wa Serikali na madhehebu ya dini ikiwemo ya wakristo jambo ambalo sio tu linasaidia kujenga uhusiano mwema miongoni mwa jamii, bali pia kueneza mafundisho sahihi ya Mtume Mtukufu S.A.W ambaye alishirikiana na waumini wa dini zingine hususan wakristo katika masuala ya imani.

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

MapenziyaMungu

Rabiul 1/ Rabiul 2 1437 AH | JANUARI 2016 | Sulh 1394 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w

Imesimuliwa na Hadhrat Abu Huraira r.a. ya kwamba Mjumbe wa Allah s.a.w. alisema: Mwenye nguvu si yule anayeshinda katika mieleka; bali mwenye nguvu hasa ndiye yule anayejitawala wakati anapoghadhibika. (*Bukhari*)

MKUTANO WA 124 WA MWAKA WA QADIAN:

Sauti ya Khalifa wa zama ni alama ya umoja

• *Khalifa Mtukufu ahutubia zaidi ya Washiriki 24,000 Qadian na London*

Na Mwandishi wetu,
Dar es Salaam

Kiongozi wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya Duniani, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (a.t.b.a) amesema kuwa sauti ya Khalifa wa zama inaashiria umoja uliopo miongoni mwa Waislamu Waahmadiyya duniani kote.

Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (a.t.b.a) ambaye ni Khalifa wa Tano wa Jumuiya ya Waislam Ahmadiyya duniani alibainisha hayo tarehe 28 Desemba, 2015 alipokuwa akitoa hotuba ya kufunga Jalsa Salana ya 124 ya Qadiani, India akiwa jijini London.

Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alihutubia kwa njia ya satellite kutoka katika msikiti wa Baitul Futuh, London ambapo zaidi ya watu 19,000 kutoka katika nchi 44 walihudhuria Jalsa huko Qadian huku watu zaidi ya 5000 wakikusanyika jijini London.



Washiriki wa Jalsa ya 124 Qadian 2015, ambapo zaidi ya watu 19,000 kutoka nchi 44 walihudhuria.

Hadhrat Mirza Masroor Ahmad, Khalifa Mtukufu V (a.t.b.a), akihutubia Jalsa Salana ya Qadian akiwa katika Msikiti wa Baitul-Futuh, London.

Waumini wakiwa katika msikiti wa Baitul Futuh, London wakimsikiliza Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) akihutubia Jalsa Salana ya Qadian.

Waumini wakiwa Qadian, wakimsikiliza Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) akihutubia Jalsa Salana moja kwa moja kutoka London.

Waumini wakiwa Qadian, wakimsikiliza Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) akihutubia Jalsa Salana moja kwa moja kutoka London.

Akishukuru juu ya fadhili hizi za Allah, Kiongozi huyo wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya Duniani alisema kuwa kwa kutumia njia za teknolojia ya kisasa ujumbe wa Masihi Aliyeahidiwa a.s umeweza kusambaa kote duniani na kwa haraka.

"Kwa fadhili za Allah, Jalsa Salana ya Qadian inamalizika leo na mimi nikiwa hapa London

Endelea uk. 11

Maisha Yangu katika Utumishi wa Jamaat Afrika Mashariki - Sheikh Chaudhry Inayatullah Ahmad

Imeandikwa na Sheikh Chaudhry Inayatullah Ahmad na kufasiriwa kutoka Kiurdu na Sheikh Yusuf Kambaulaya



Sheikh Inayatullah Ahmad akiwa kwenye picha ya pamoja na kijana wake Bw. Muhammad Saidi Manoro wakati alipomtembelea London mwaka 2008

Mtumishi huyu Choudhry Inayatullah Ahmadi nilizaliwa tarehe moja Januari mwaka 1920 (01/01/1920) katika mji wa Amritsar Punjab nchini India. Baba yangu Hadhrat Choudry Allah Bakhshi sahib alikuwa ni sahabi wa Hadhrat Masihi Mauud (as) huyu alikuwa anamiliki mtambo wa kupigia chapa kwa kutumia mvuke mjini Qadian. Baba alitupeleka Qadian kwa ajili ya masomo mimi nilikuwa na miaka mitano (5). Mwaka 1934 Hadhrat Muslih Mauud (ra) alipotoa hotuba ya Ijumaa kuwa vijana wa Kiahmadiyya watoke majumbani mwao na kwenda nje –ng'ambo. Basi mimi nikaweka nia kuwa baada ya kufaulu mtihani wa darasa la kumi (Martirculation) kwa ajili ya kuitumikia dini nitatoka nyumbani na kwenda kwenye nchi yoyote ile.

Mwaka 1935 nilifaulu masomo yangu ya Martirculation na nikaanza kufanya kazi katika kiwanda cha baba yangu cha kupigia chapa nikiwa ndiyo Meneja wa kiwanda. Tarehe 22 Oktoba 1938 niliondoka Qadian kuelekea Afrika Mashariki na tarehe 05 Novemba 1938 nikawasili katika mji wa Mombasa na nikafikia kwa Marehemu Babu Muhammad Alim sahib Rais wa Jamaat ya Mombasa. Jioni yake niliondoka kuelekea Uganda ambako Shemeji yangu mheshimiwa Dr. Ahmad Din sahib aliyekuwa anafanya kazi ya Udaktari mjini Kamuli alinipokea vizuri. Mwanzoni mwa mwaka 1939 Kamishna Mkuu wa Polisi wa Uganda aliyekuwa Mwingereza baada ya kunikuta kwa Dr. Ahmad Din sahib akamwambia Dokta kuwa mlete nduguyo huyu kwangu Polisi na mimi siku ya kwanza tu nitamwajiri na kumpa cheo cha Inspector wa Polisi. Baada ya kufanya maombi ya Istikhara nikaikataa kazi hii ya Polisi na nikamwambia kuwa mimi nimejipangia kuitumikia dini na niliendelea kufanya mahubiri katika eneo la KAMULI.

MWAKA 1939 KATIKA HOTUBA MOJA YA Ijumaa Hadhrat Muslih Mauud (ra) akasema kuwa vijana wa Kiahmadiyya wanatakiwa wajiunge na jeshi la ulinzi ili wasaidie mataifa yao. Baada ya kusoma maagizo hayo mimi nikajiunga na jeshi la ulinzi nchini Uganda. Kwanza 1940 nilienda Nairobi kisha nikaenda Moshi Tanzania. 1940 nikiwa Moshi nilipata fursa pia ya kiufanya mahubiri huko na kwa njia hii nikaendeleza mahusiano na nchi ya Tanzania. Kutoka Moshi nikapelekwa Jinja, huko pia kwa fadhili za Allah niliendelea kufanya mahubiri. Wakati huo Moshi hakukuwa na Jamaat na hata Jinja pia kulikuwepo nyumba mbili tatu tu za Wanajumuiyya wenye asili ya Kiasia. Mwaka 1941 wakati wa likizo nikaenda Tabora. Kwa maagizo ya Maulana Sheikh Mubarak Ahmad Raisultabligh Afrika Mashariki nikasalisha sala ya Ijumaa. Maulana Sheikh Mubarak sahib mara mbili kwa wiki alikuwa akiwafundisha elimu ya dini wanafunzi wa Kiislam wa Tabora School kwa masaa mawili. Siku moja nikaagizwa niwahutubie wanafunzi hao mambo ya dini. Huku nikiambatana na Maulana Sheikh sahib. Nikaenda Shuleni hapo

Endelea uk. 10